Ukatili wa Kingono:

Tishio kwa Haki na Ustawi wa Mtoto nchini Tanzania

# MUHTASARI WA RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU 2018

TANZANIA BARA

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kimetayarishwa na:

Bw. Fundikila Wazambi na Bi. Joyce Komanya

Kimehaririwa na:

Bi. Anna Henga (Wakili)
Bi. Felista Mauya
Bw. Fulgence Massawe (Wakili)
Bi. Naemy Sillayo (Wakili)
Bw. Paul Mikongoti

Kimechapishwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

Aprili, 2019

*Kitabu hiki hakiuzwi*

ISBN: 978-9987-740-48-2

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| KUHUSU KITUO CHA SHERIA CHA HAKI ZA BINADAMU (LHRC) | i |
| UTANGULIZI | ii |
| SURA YA KWANZA: KUHUSU TANZANIA | 9 |
| SURA YA PILI: HAKI ZA KIRAIA | 12 |
| SURA YA TATU: HAKI ZA KISIASA | 18 |
| SURA YA NNE: HAKI ZA KIUCHUMI | 20 |
| SURA YA TANO: HAKI ZA KIJAMII NA KIUTAMADUNI | 24 |
| SURA YA SITA: HAKI ZA KIUJUMLA | 26 |
| SURA YA SABA: HAKI ZA MAKUNDI MAALUM | 28 |
| SURA YA NANE: RUSHWA, UTAWALA BORA NA HAKI ZA BINADAMU | 38 |
| SURA YA TISA: MFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU | 39 |
| SURA YA KUMI: MASUALA MENGINE YANAYOATHIRI HAKI ZA BINADAMU | 42 |
| MATATIZO YA JUMLA YANAYOATHIRI ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU | 34 |
| MAPENDEKEZO MUHIMU | 43 |
| HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA | 35 |
| HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI | 36 |
| HAKI ZA MAKUNDI MAALUM | 39 |

# KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC)

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilo la kiserikali, lisilofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu ambao wapo kwenye hatari kubwa ya kunyimwa haki zao za msingi, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

UTANGULIZI

## Matukio Makubwa yaliyogusa Ulinzi wa Haki za Binadamu kwa mwaka 2018

Ongezeko kubwa la matukio ya ukatili dhidi ya watoto

Waziri wa Mambo ya Ndani kuamrisha polisi kutoa dhamana kwa watuhumiwa siku za mwisho wa juma na kutoa onyo dhidi ya askari wanaowabimbikia watu kesi

Muswada wa Kanuni zenye utata za Maudhui ya Mtandaoni kupitishwa na kusainiwa kuwa sheria

Serikali kuanzisha madawati ya jinsia katika shule za msingi na sekondari kama sehemu ya kukuza utoaji taarifa na kupambana na ukatili dhidi ya watoto

Maafisa wa Mgodi wa North Mara kutuhumiwa kutoa rushwa kwa watendaji wa Serikali na kufikishwa mahakamani

Kuletwa kwa Muswada wenye utata wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992

Taarifa kuhusu matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenzao mashuleni

Viongozi wa ngazi za juu serikalini kukemea matumizi mabaya ya mamlaka ya wakuu wa mikoa na wilaya ya kukamata na kuwaweka kuzuizini watu

Tanzania kushuka katika viwango vya uhuru wa vyombo vya habari duniani

Mhimili wa Mahakama kuchukua hatua mbalimbali kuboresha upatikanaji haki na kupambana na ukatili dhidi ya watoto

Uhaba mkubwa wa madarasa kwa wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba na kufaulu kuingia elimu ya sekondari

Kutekwa kwa mfanyabiashara mkubwa jijini Dar es Salaam, kukileta wasiwasi kuhusu hali ya usalama wa mtu Tanzania Bara

Kushamiri kwa mauaji ya wazee katika mikoa ya Tabora, Songwe, Kagera na Rukwa

Kuuwawa kwa mwanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Akwelina Akwilini, wakati wa maandamano ya chama cha siasa jijini Dar es Salaam

Wadau wa kitaifa na kimataifa waonyesha wasiwasi kuhusu kushuka kwa ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania

Wasiwasi kuhusiana na gharama za chaguzi ndogo za marudio kufuatia hamahama katika vyama vya siasa nchini Tanzania

Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141, ambayo yanazitaka mahakama kutofungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi katika kutoa maamuzi katika kesi au mashauri ya madai au jinai, ili kuhakikisha haki inatendeka

Kushamiri kwa matukio ya madereva bodaboda kutekwa na kuuwawa

Kutungwa kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018

Kutungwa kwa Marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2018

Kuletwa na kuondolewa kwa muda kwa kikokotoo kipya cha malipo ya pensheni ya wastaafu

Kutungwa kwa Kanuni za Utoaji wa Msaada wa Kisheria za mwaka 2018

# Haki 5 zilizovunjwa zaidi mwaka 2018



1. **Uhuru dhidi ya Ukatili**
   Ukatili wa kingono dhidi ya watoto;
   Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto;
   Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake;
   Ukatili dhidi ya wazee; na
   Ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya wanawake

2. **Haki ya Kuishi**
   Kujichukulia sheria mkononi;
   mauaji yanayotokana na imani za kishirikina;
   mauaji ya wazee
   mauaji yanayofanywa na maafisa wa vyombo vya dola;

3. **Uhuru wa Kujieleza**
   Kuminywa kwa uhuru wa kujieleza
   Kutokana na kuwepo kwa sheria zenye
   Vifungu kandamizi; unyanyasaji na
   Upigaji wa wanahabari

4. **Haki ya Kuwa Huru na Salama**
   Ukamataji na uwekaji watu kiuzini
   Kinyume na sheria; matukio ya utekaji;
   Mauaji (mfano ya wazee)

5. **Uhuru wa kukusanyika na Kujumuika**
   Kuminywa kwa uhuru wa kukusanyika;
   Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria
   ya Vyama vya Siasa, ambayo
   yameonekana kuminya kwa kiasi
   kikubwa uhuru wa vyama vya siasa
   kufanya shughuli za kisiasa

# Madhumuni ya Ripoti na Ukusanyaji Taarifa

Lengo kubwa la ripoti hii ni kuelezea hali ya haki za binadamu kwa mwaka 2018, ikionyesha ukiukwaji wa haki hizo na jitihada zilizofanywa kuzilinda. Pia, lengo la ripoti hii ni kulinganisha hali za haki za binadadamu katika miaka ya 2018 na 2017; na pia kutumika kama nyenzo ya utetezi na kujifunzia haki za binadamu.

Taarifa zilizotumika kuandaa ripoti hii zilikusanywa kwa njia mbalimbali, ikiwemo kutoka:

Taasisi mbalimbali za Serikali;
Mahakama;
Bunge;
maafisa katika halmashauri mbalimbali nchini;
Jeshi la Polisi;
waangalizi wa haki za binadamu;
asasi nyingine za kiraia zilizopo Tanzania Bara;
mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kimataifa;
wateja wa msaada wa kisheria;
wasaidizi wa kisheria;
vyombo vya kitaifa na kimataifa vinavyosimamia haki za binadamu; na vyombo vya habari.

Ripoti hii imeandaliwa kwa kutumia taarifa za matukio na masuala yaliyotokea mwaka 2018 zilizokusanywa kuanzia mwezi Januari 2018 hadi mwezi Machi 2019.

# Muundo wa Ripoti

Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania 2018 imegawanyika katika sehemu 2. Sehemu ya Kwanza inaonyesha hali ya haki za binadamu kwa upande wa Tanzania Bara, huku sehemu ya pili ikionyesha hali ya haki za binadamu kwa upande wa Zanzibar. Sura ya Kwanza inaelezea kuhusu Tanzania kama nchi, ikugusia kwa ufupi historia, jiografia, idadi ya watu na mihimili ya dola.

Sura za Pili hadi Sita zinaelezea haki mbalimbali za binadamu, ambazo ni za kiraia na kisiasa; kiuchumi, kijamii na kiutamaduni; na kiujumla. Sura ya Saba imejikita katika haki za makundi maalum, ambayo ni wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Sura ya Nane inaelezea madhara ya rushwa kwenye haki za binadamu, wakati Sura ya Tisa inaelezea mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu. Sura ya mwisho ni Sura ya Kumi, ambayo inaelezea masuala mengine ambayo yaligusa au kuathiri haki za binadamu mwaka 2018.

# Mikoa ya Kuiangalia

| Mkoa | Masuala ya Kuangaliwa zaidi |
|---|---|
| Mwanza | Ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya watoto<br>Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina |
| Tabora | Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina<br>Ukatili wa kiuchumi na kisaikolojia dhidi ya wanawake<br>Ndoa za utotoni<br>Mimba za utotoni |
| Dar es Salaam | Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto<br>Kujichukulia sheria mkononi<br>Uhuru wa kujieleza |
| Kilimanjaro | Ukatili wa kiuchumi na kingono dhidi ya wanawake<br>Ukatili wa kingono dhidi ya watoto |
| Mbeya | Ukatili wa kingono dhidi ya watoto<br>Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake |
| Iringa | Ukatili wa kingono dhidi ya watoto<br>Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake |
| Shinyanga | Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina<br>Ndoa za utotoni |
| Singida | Ukatili wa kingono dhidi ya watoto<br>Ukatili wa kiuchumi dhidi ya wanawake |
| Kigoma | Ukatili wa kingono dhidi ya wanawake |

## 1.1. Historia

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza katika Karne ya 19, Tanganyika (sasa Tanzania Bara) ilikaliwa na wazawa waliokuwa wakizungumza lugha ya Kibantu, ambao baadae walipata ugeni toka Bara la Asia na toka Uarabuni. Kufikia Karne ya 15 Wareno nao wakaingia; na katika kipindi hicho cha Waarabu na Wareno, ndipo biashara ya utumwa ilipamba moto. Ilipofika mwaka 1880 ulifanyika mkutano mkubwa katika Mji wa Berlin – Ujerumani, ambapo nchi za Ulaya ziliirigawa Bara la Afrika kwa ajili ya kulitawala. Ujerumani ilipewa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanganyika.


Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya ukoloni wa Uingereza, mpaka ilipofikia mwaka 1961, ambapo Tanganyika ilipata uhuru. Katika kipindi chote cha ukoloni, machifu mbalimbali walipigana na uongozi kandamizi wa kikoloni, ambao ulikandamiza haki zao kama binadamu, akiwemo Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi, Mangi Meli wa Wachagga na Abushri wa Pangani. Mapigano makubwa zaidi yalitokea Mwaka 1905 wakati wa ukoloni wa Mjerumani, yakifahamika zaidi kama Vita vya Majimaji, ambavyo viliongozwa na kiongozi wa kimila na kiroho aliyeitwa Kinjekitile Ngwale, ambaye aliaminika kuwa na uwezo wa kugeuza risasi kuwa maji.

Harakati za kupata uhuru ziliongozwa na chama cha TANU (Tanganyika African National Union), ambacho kilizaliwa mwaka 1954, kabla ya hapo kikifahamika kama TAA (Tanganyika African Association), kilichoanzishwa mwaka 1929. Kiongozi wa chama alikuwa Mwl. Julius Nyerere, ambaye aliiongoza TANU na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza chini ya Katiba ya Uhuru. Mwaka 1962, Tanganyika ikawa Jamhuri, Nyerere akiwa Rais wake wa kwanza chini ya Katiba ya Jamhuri, ambayo ilimfanya kuwa Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, pia akiwa sehemu ya Bunge. Mwaka 1964, Tanganyika iliungana na Zanzibar, ambayo ilikuwa imepata uhuru toka kwa Sultani wa Oman mwaka 1963, na kuunda Tanzania.

Katiba ya tatu, Katiba ya Muungano, iliundwa, ikileta mfumo wa serikali mbili, chini ya vyama vya TANU (Tanzania Bara) na ASP (Zanzibar). Mwaka 1965, Katiba ya Mpito iliundwa, ambayo ilirudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja. Katiba hii ilipitishwa kama sheria nyingine za bunge, kinyume na kanuni za kikatiba. Mwaka 1977, vyama vya siasa vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilitengeneza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo ndio inayotumika mpaka leo, japo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali yapatayo kumi na nne mpaka mwaka 2015.

Mojawapo ya marekebisho makubwa ni yale ya mwaka 1992, ambayo yalirudisha mfumo wa vyama vingi. Mengine ni yale ya mwaka 1984, ambayo hatimaye yaliingiza hati ya haki za binadamu kwenye Katiba. Kabla ya hapo, tangu nchi ipate uhuru, haki za binadamu hazikuonekana kuwa muhimu sana kuwekwa kwenye Katiba, japo Tanzania ilikuwa imeshaanza kuridhia baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

## 1.2. Jiografia



Tanzania iko kati ya Latitudo 10 na 120 Kusini na Longitudo 290 na 410 Mashariki. Inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia kwa pande nyingine. Tanzania ndio nchi kubwa kuliko zote Afrika Mashariki na kuna Mlima Kilimanjaro, ambao ndio mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, wa tatu duniani. Tanzania imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi, ikiwemo mimea, mabonde ya ufa, maziwa, mito na mbuga za wanyama. Maziwa ni pamoja na Ziwa Victoria - ambalo ni kubwa kuliko yote Afrika, na Ziwa Tanganyika - ambalo lina kina kirefu kuliko yote Afrika. Mbuga za wanyama ni pamoja na Serengeti, Mikumi, Manyara, Ngorongoro na Katavi.

## 1.3. Idadi ya watu


Idadi ya watu Tanzania inaendelea kuongezeka, ambapo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 43,625,354 kwa Tanzania Bara na 1,303,569 kwa Zanzibar. Wanawake ni wengi zaidi (51.3%) ukilinganisha na wanaume (48.7%). Kufikia mwaka 2016, idadi ya watu iliongezeka hadi kufikia takribani 50,144,175, huku 24,412,889 wakiwa wanaume na 25,731,286 wakiwa wanawake. Idadi kubwa ya watu wapo vijijini kuliko mijini

## 1.4. Mihimili ya Dola

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

### A. Serikali

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania unautumia, na ina mamlaka juu mambo yote ambayo sio ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



| Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | |
|---|---|
| Mw. Julius Kambarage Nyerere | 1964-1985 |
| Ali Hassan Mwinyi | 1985-1995 |
| Benjamin William Mkapa | 1995-2005 |
| Jakaya Mrisho Kikwete | 2005-2015 |
| John Pombe Magufuli | 2015- mpaka sasa |

## B. Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio chombo kikuu cha kutengeneza sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala (CCM) na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambacho ndio chombo chake kikuu cha kutengeneza sheria na kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa

## C. Mahakama

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchiniTanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufaa, ambayo ina majaji wa Mahakama ya Rufaa, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndio mahakama ya chini kabisa. Tofauti na mahakama za rufaa na kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi na kingine kipya cha rushwa – ambacho kimeundwa hivi karibuni (mwaka 2016). Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna Mahakama Maalum ya Katiba, ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufaa ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufaa ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

# SURA YA PILI:

# HAKI ZA KIRAIA

## Utangulizi

Haki za kiraia zinalindwa kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pia inajumuisha haki za binadamu, zikiwemo haki za kiraia. Ripoti hii imejikita katika haki muhimu sita, ambazo ni Haki ya Kuishi, Uhuru wa Kujieleza, Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria, Haki ya Kuwa Huru na Usalama wa Mtu na Haki ya Kutoteswa. Hivyo, haki hizi zinalindwa katika ngazi za kitaifa na kimataifa na ni haki muhimu katika ufurahiaji wa haki nyingine za binadamu.


Kwa ujumla, hali ya haki za kiraia na kisiasa kwa mwaka 2018 ilidorora zaidi kiasi ikilinganishwa na mwaka 2017. Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na uminywaji wa haki za uhuru wa kujieleza; ukiukwaji wa haki ya kuwa huru na salama na uhuru dhidi ya utesaji; na uminywaji wa uhuru wa kujumuika na haki ya kushiriki katika utawala.

| Haki Zilizoangaliwa (5) |
| --- |
| Haki ya Kuishi,<br>Uhuru wa Kujieleza,<br>Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria,<br>Haki ya Kuwa Huru na Usalama wa Mtu,<br>Haki ya Kutoteswa |

## 2.1. Haki ya Kuishi


Ripoti hii imejikita katika matukio ya kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola, ukatili dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, adhabu ya kifo na ajali za barabarani kama masuala makuu yaliyoathiri haki ya kuishi kwa mwaka 2018. Hata hivyo, haki ya kuishi ndio haki ya msingi kuliko zote na ukiukwaji wa haki nyingine za msingi za binadamu pia uliathiri haki hii. Matukio mengine yaliyoathiri haki ya kuishi kwa mwaka 2018 ni pamoja na: ukiukwaji wa haki za walaji kupitia uingizwaji na usambazaji wa bidhaa feki, ikiwemo vyakula; utekaji na mauaji; vitendo vya ukatili dhidi ya watu mbalimbali, ikiwemo ukatili wa kingono na kimwili; mauaji ya askari polisi mkoani Kigoma; na kutotekelezwa kwa haki za kijamii na kiuchumi.

Kwa mwaka 2018, hali ya haki ya kuishi iliimarika kiasi ikilinganishwa na mwaka 2018. Hii inatokana na kupungua kiasi kwa matukio ya mauaji




# Mauaji yayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, 2014-2018

Chanzo: Takwimu za Matukio ya Uhalifu za Jeshi la Polisi




# Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, 2014-2018

Chanzo: Takwimu za Matukio ya Uhalifu za Jeshi la Polisi

yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na matukio ya ajali za barabarani vifo vinavyotokana na ajali hizo. Hata hivyo, idadi za matukio haya bado ni kubwa na yanaendelea kuwa tishio kubwa kwa haki ya kuishi.

Kujichukulia Sheria Mkononi: Wastani wa watu 65 waliuwawa kutokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi ('wananchi wenye hasira kali') katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni mwaka 2018. Matukio haya bado yameendelea kutokea zaidi maeneo ya mijini. Jumla ya matukio 385 ya mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi yaliripotiwa katika vituo vya polisi katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2018. Kutokuwa na imani na vyombo vya haki (polisi na mahakama) kumeendelea kuwa sababu kubwa ya utekelezaji wa mauaji ya aina hii, huku uelewa mdogo kuhusu sheria na taratibu zake pia ukichangia.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaona kwamba imani juu ya vyombo vya haki bado iko chini miongoni mwa wananchi wengi, na inachangiwa na tatizo la rushwa katika vyombo hivyo. Wakati mwingine, kama ilivyoelezewa hapo juu, uelewa mdogo kuhusu sheria na taratibu zake, mfano utaratibu wa kutoa dhamana, unachangia wananchi kuona hakuna haki itakayotendeka na kuamua kujichukulia sheria mkononi.

Mauaji yanayofanywa na Vyombo vya Dola na Ukatili dhidi ya Maafisa wa Vyombo hivyo: Kwa mwaka 2018, LHRC ilikusanya matukio matano (5) ya mauaji yaliyofanywa na maafisa wa vyombo vya dola, ambayo ni matukio manne (4) pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2017. Matukio haya yaliripotiwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mara, Mbeya, Tanga na Tabora. Mauaji haya hutokea pale ambapo maafisa wa vyombo vya dola wametumia nguvu kupita kiasi na utesaji wa mtuhumiwa mpaka kupelekea kifo chake. Kwa upande mwingine, LHRC ilikusanya matukio mawili ya ukatili dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola, ambapo maafisa wawili wa polisi, akiwemo Inspekta Ramadhani Mbini, waliuwawa katika Kijiji cha Mpeta, Wilaya ya Uvinza – mkoani Kigoma, wakati wakifanya operesheni ya kuwaondoa wafugaji katika kijiji hicho.

Mauaji yanayotokana na Imani za Kishirikina na Ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi: Jumla ya mauaji 106 yanayotokana na imani za kishirikina yaliripotiwa katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2018. LHRC ilikusanya matukio ya mauaji haya

kutoka mikoa ya Tabora, Geita, Morogoro, Songwe, Rukwa, Mwanza, Ruvuma na Shinyanga. Kwa upande wa watu wenye ulemavu wa ngozi, wamekuwa wakishambuliwa na kuuwawa kwa ajili ya kutumia viungo vyao kwenye imani za kishirikina, japo matukio haya yamepungua kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni kutokana na juhudi mbalimbali za wadau mbalimbali, wakiongozwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa mwaka 2018, LHRC ilipata taarifa kuhusu tukio moja la njama za kumshambulia mtu mmoja mwenye ulemavu wa ngozi katika kilabu cha pombe mkoani Singida, ambapo msamaria mwema alimtonya kuhusiana na njama hizo na kumwezesha kukimbia. Pamoja na kupungua kwa matukio ya kushambuliwa kwao, watu wenye ulemavu wa ngozi waemeendelea kuishi kwa hofu, hasa katika kipindi kama hichi ambapo nchi inaelekea katika chaguzi kubwa mbili za mwaka 2019 na 2020.

Adhabu ya Kifo: Kwa mwaka 2018, LHRC ilikusanya jumla ya matukio matano ya hukumu za vifo, ambayo ni machache zaidi ulinganisha na matukio 15 yaliyoripotiwa mwaka 2017. Kwa sasa, kuna wafungwa zaidi ya 480 ambao wanasubiri kunyongwa, wengi wao (90%) wakiwa wanaume.

Ajali za Barabarani: Ajali za barabarani zimeendelea kupungua tangu mwaka 2016. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2018, matukio 2,220 ya ajali na vifo 1,051 viliripotiwa, ukilinganisha na ajali 3,090 na vifo 1,308 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017.


## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Uhuru wa kujieleza ni haki ya msingi ya binadamu. Uhuru huu unajumuisha uhuru wa vyombo vya habari, haki ya kupata taarifa na uhuru wa kutoa maoni.

Kwa mwaka 2018, hali ya uhuru wa kujieleza iliendelea kudorora, kutokana na uminywaji wa haki hizo, ambao uliathiri na utaendelea kuathiri shughuli za asasi za kiraia, watetezi wa haki za binadamu, vyama vya siasa, vyombo vya habari na uhuru wa wanajamii kwa ujumla.

Uminywaji huu wa uhuru wa kujieleza umechangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa nafasi ya ushiriki nchini Tanzania. Mambo makubwa yaliyoathiri uhuru wa kujieleza kwa mwaka 2018 ni:

Kupitishwa kwa Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni, ambazo zimekuwa tishio kwa uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kutoa maoni na haki ya kupata taarifa. Vifungu vya kanuni hizi ambavyo vimeonekana kuminya uhuru wa kujieleza ni pamoja na: makatazo na fasili ambazo hazijitoshelezi ama kueleweka vizuri; wamiliki wa biashara ya mtandao kutakiwa kuweka kamera za video na




Matukio ya ajali na vifo, 2016-2018

### Masharti ya Upatikanaji Haki

Uwepo wa mahakama zilizo huru na zisizoegemea upande wowote

Uwepo wa sheria nzuri

Mahakama kuweza kufikika kirahisi na wanajamii na kuwa na rasimali za kutosha kuhakikisha upatikanaji wa haki

Uwepo wa wanasheria wenye vigezo kwa ajili ya kutoa uwakilishi wa kisheria

Kesi kuendeshwa kwa haki na kwa muda mfupi kadri itakavyowezekana (haki kutochukua muda mrefu kupatikana)



kurekodi shughuli za watumiaji wa mtandao na kuhifadhi rekodi hizo kwa takribani mwaka mmoja; adhabu kali na zinazofanana kwa makosa mbalimbali yaliyoainishwa kwenye kanuni hizo; kutoa mamlaka makubwa kupita kiasi kwa mamlaka ya usimamizi; wamiliki wa blogu na vyombo vingine katika mtandao kutakiwa kujisajili, kupewa leseni na kulipa ada kila mwaka; jukumu la kurekebisha na kuchuja maudhui; baadhi ya majukumu ya waombaji wa leseni za utoaji huduma za mtandao; na baadhi ya majukumu ya wasimamizi wa maudhui ya mtandaoni.

Bugudha na vitisho kwa wanahabari/waandishi wa habari: LHRC ilikusanya takribani matukio manne ya bughudha kwa wanahabari, ikiwemo wanahabari kutoka Kamati ya Kuwalinda Wanahabari (CPJ) na kupigwa kwa mwandishi wa habari wakati wa tamasha la michezo ndani ya Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015: Wasiwasi mkubwa kuhusiana na marekebisho hayo ni pamoja na: katazo la kutochapishwa takwimu ambazo zinazokinzana au kupotosha takwimu rasmi za Ofisi ya Taifa ya Takwimu; na kutochapisha baadhi ya takwimu bila ridhaa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Kuendelea kutumika kwa sheria kama Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, ambazo zina vifungu vinavyominya uhuru wa kujieleza kinyume na Katiba na mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu.

Waajiri kuwabana waajiriwa katika kufurahia haki ya uhuru wa kujieleza: LHRC ilipokea malalamiko kadhaa kuhusu waajiri kuwabana waajiriwa wao kuhusiana na uhuru wao wa kutoa maoni ambayo wao 'wanaona hayafai.'

Mazingira magumu ya kazi ya uandishi wa habari kutokana na hofu juu ya sheria mbalimbali na bughudha kwa wanahabari, ikiwemo vitisho kutoka kwa watu wasiojulikana. Suala hili linawafanya wasiwe huru kuandika baadhi ya habari na kutopata ushirikiano kutoka kwa wananchi wanapoomba maoni yao kuhusu habari fulani wanayoandaa. Utafiti uliofanywa na Shirika la Twaweza mwaka 2018 unaonyesha kwamba asilimia 62 ya wananchi wanaona kwamba uhuru wa vyombo vya habari kuripotia makosa ya serikali umepungua.




## 2.3. Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria

Haki ya usawa mbele ya sheria inajumuisha: upatikanaji wa haki, haki ya uwakilishi wa kisheria na haki ya kesi/mashauri kuendeshwa kwa haki. Haki ya nafuu madhubuti ya kisheria ni haki ya msingi inayohusiana na haki ya usawa mbele ya sheria.

Kwa mwaka 2018, haki za usawa mbele ya sheria na nafuu madhubuti za kisheria ziliimarika kiasi kufuatia hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali na Mhimili wa Mahakama ili kuongeza upatikanaji na ufikiaji wa haki na nafuu za kisheria. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kufanya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Rufaa, Sura ya 141, ambayo yanazitaka mahakama kutofungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi katika kutoa maamuzi katika kesi au mashauri ya madai au jinai, ili kuhakikisha haki inatendeka; kutungwa kwa Kanuni za Utoaji wa Msaada wa Kisheria za mwaka 2018; uajiri wa watumishi wapya katika sekta ya mahakama; utekelezaji wa sera ya Mhimili wa Mahakama ya kupunguza mlundikano wa kesi; kuletwa kwa mpango wa mahakama zinazotembea ili kurahisisha ufikiaji haki; na ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama.

Hata hivyo, utekelezaji na ufurahiaji wa haki hizi uliendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo: rushwa kwenye mfumo wa haki; ukiukwaji wa haki za watuhumiwa; uhaba wa rasilimali kwenye Mhimili wa Mahakama; na gharama kubwa za kupata uwakilishi madhubuti wa kisheria.



Upatikanaji uliendelea kuathiriwa na changamoto kadhaa, ikiwemo: msaada wa kisheria kwa watu wa hali ya chini kutopatikana kirahisi katika baadhi ya maeneo; rushwa kwenye mfumo wa haki; vituo vya polisi na mahakama kuwa mbali; gharama kubwa za uwakilishi madhubuti wa kisheria; uelewa mdogo kuhusu sheria na taratibu mbalimbali za kisheria miongoni mwa wanajamii; uhaba wa wanasheria/mawakili; na uwekwaji kizuizini kwa muda mrefu kinyume na sheria. Mambo mengine yaliyoathiri ufurahiaji wa haki hizi ni pamoja na: mawakili wa watuhumiwa kutishiwa; kuingilia uhuru wa mahakama; watu wengi kuwa jela kwa muda mrefu kama watuhumiwa wa makosa ya jinai kabla ya hukumu kutolewa; uwepo wa wanasheria wasio na maadili ambao wanaowadhulumu wateja; tatizo la Lugha ya Kiingereza kwa mawakili na mahakimu wengi; uhaba wa watumishi; rushwa; na bajeti finyu kwa ajili ya posho za wazee washauri wa mahakama katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo, sambamba na ucheleweshaji wa fedha hizo. Kwa mujibu wa Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Hamis Juma, kuna hitaji la watumishi 24,643 kwenye sekta ya mahakama lakini idadi iliyopo ni watumishi 6,096.

Kwa mwaka 2018, haki za kesi kuendeshwa kwa haki na nafuu madhubuti ya kisheria ziliendelea kuathiriwa na: kutoweza kufikia mahakama kirahisi na ucheleweshaji katika uchunguzi na uendeshaji wa kesi. Makadirio ya hivi karibuni yanaonyesha kwamba zaidi ya Watanzania milioni 20 hawawezi kuifikia Mahakama Kuu kupata haki. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, ucheleweshaji na taratibu ndefu au zisizo za lazima katika mfumo wa haki zinaigharimu Tanzania wastani wa Dola za Kimarekani Milioni 464 kwa mwaka.

Pia, rushwa imeendelea kuwa adui wa haki na kikwazo katika ufurahiaji wa haki za kesi/mashauri kuendeshwa kwa haki na nafuu ya kisheria. Rushwa imeendelea kushamiri zaidi katika mahakama za chini, ambazo ndizo Watanzania wengi wanaweza kuzifikia.



### 2.4. Haki ya Kuwa Huru na Salama

Kwa mwaka 2018, haki ya kuwa huru na salama iliathiriwa na ukamataji kinyume na sheria, ikiwemo amri za ukamataji na uwekaji kizuizini zinazotolewa na wakuu wa mikoa na wilaya; mauaji yenye utata; na matukio ya utekaji.

Uhuru wa Kutokamatwa na Kuwekwa Kizuizini kinyume na sheria: Matukio mbalimbali ya ukiukwaji wa uhuru wa kutokamatwa na kuwekwa kizuizini kinyume na sheria yaliripotiwa mwaka 2018, ikiwemo: kukamatwa kwa mwandishi wa habari jijini Dar es Salaam; na kukamatwa na kuwekwa kizuizini kinyume na sheria kwa mwanafunzi wa chuo kikuu, Abdul Nondo. Pia, katika mwaka huo kulitokea malalamiko mengi ya polisi kuwabambikizia watu kesi, hali ambayo ilipelekea Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Kangi Lugola, kutoa onyo kali dhidi ya askari wanaofanya vitendo hivyo. Amri za ukamataji na uwekaji watu kizuizini kinyume na sheria pia zilikuwa gumzo mwaka 2018, ambazo zilikemewa na viongozi kadhaa wa ngazi za juu serikalini, akiwemo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mh. Selamani Jafo.

Haki ya Usalama wa Mtu: Matukio ambayo yalikuwa tishio na kuleta wasiwasi kuhusiana na haki ya usalama wa mtu ni pamoja na: mauaji ya mwanaharakati wa masuala ya ardhi, Godfrey Luena, mkoani Morogoro; mashambulizi na mauaji ya afisa wa chama kimoja cha upinzani jijini Dar es Salaam; utekaji wa mfanyabiashara mkubwa jijini Dar es Salaam; mauaji ya polisi wilayani Uvinza, mkoani Kigoma; na utekaji wa mwanafunzi wa chuo kikuu. Suala jingine ni kuongezeka kwa matukio ya utekaji na mauaji ya madereva bodaboda katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. Pia, matukio kama vile upoteaji wa mwanasiasa Ben Saanane tangu mwaka 2016 na mwandishi wa habari Azory Gwanda tangu mwaka 2017, pamoja na shambulio la risasi kwa mbunge Tundu Lissu, pia mwaka 2017, bado hayajapatiwa majibu.

Haki ya Kupata Dhamana: Japokuwa haki ya kupata dhamana inalind wa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki hiyo, hasa inayotolewa katika vituo vya polisi, ilikuwa mojawapo ya haki za msingi zilizokiukwa mwaka 2018. Baadhi ya maaskari polisi walituhumiwa kudai fedha kutoka kwa ndugu na jamaa wa watuhumiwa kama sharti la kuwaachia kwa dhamana jamaa zao walio chini ya ulinzi wa polisi. Kutokana na malalamiko hayo, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. KangiLugola, alitoa onyo kali kwa maaskari polisi wanaojihusisha na vitendo hivyo vya rushwa na kutoa amri ya dhamana kutolewa hata wakati wa mwisho wa juma, ambapo mara nyingi imekuwa haitolewi.

### 2.5. Haki ya Kutoteswa

Kwa mwaka 2018, matukio kadhaa ya utesaji yaliripotiwa, ikiwemo: utesaji wa mwandishi wa habari wakati wa tamasha la michezo katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam; utesaji wa mfanyabiashara mmoja uliofanywa na askari mgambo baada ya kukamatwa eneo la Bunju jijini Dar es Salaam; kupigwa kwa mwandishi wa habari wilayani Tarime, mkoani Mara; na utesaji wa watoto unaofanywa na wazazi, walimu na walezi, likiwemo tukio la mwalimu mmoja mkoani Kagera kumpiga vibaya na kumchapa mwanafunzi wa shule ya msingi kwa madai ya kuiba pochi ya mwalimu na kupelekea kifo chake.

SURA YA TATU

HAKI ZA KISIASA

## Utangulizi

| Haki Zilizoangaliwa (3) |
|---|
| Uhuru wa Kukusanyika,<br>Uhuru wa Kujumuika,<br>Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali |

Kama ilivyo kwa haki za kiraia, haki za kisiasa zinalindwa kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu.

Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pia inajumuisha haki za binadamu, zikiwemo haki za kisiasa.

### 3.1. Uhuru wa Kukusanyika

Kwa mwaka 2018, uhuru wa kukusanyika uliendelea kuathiriwa na katazo la kutofanya mikutano ya hadhara nje ya jimbo ya mwanasiasa husika. Wanasiasa kadhaa wa vyama vya upinzani walikamatwa kwa kutotii katazo hili, japo halina uhalali wa kisheria; na kulikuwa na malalamiko ya maombi ya kukusanyika kukataliwa mara kwa mara na Jeshi la Polisi. Katazo la kukusanyika kinyume na sheria linakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mwongozo kuhusu Uhuru wa Kujumuika na Kukusanyika barani Afrika, na viwango mbalimbali vya kimataifa vya uhuru wa kujumuika na kukusanyika.

### 3.2. Uhuru wa Kujumuika

Ukiukwaji wa uhuru wa kukusanyika mwaka 2018 uliathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ufurahiaji wa uhuru wa kujumuika. Kama ambavyo Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilielezea katika Kesi ya Mtandao wa Kidunia dhidi ya Utesaji na wengine dhidi ya nchi ya Zaire, kutoviruhusu vyama vya upinzani kukutana na kuvibughudhi ni ukiukwaji wa haki yao ya uhuru wa kujumuika. Kwa mwaka 2018, vyama vya upinzani pia vililalamika kuhusu kutotendewa haki katika utekelezaji wa shughuli za kisiasa, ikiwemo kubughudhiwa, kunyimwa au kucheleweshewa dhamana katika kesi mbalimbali na adhabu za vifungo. Pia, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 yaliyotolewa mwaka 2018 yalitishia zaidi uhuru wa kujumuika wa vyama vya siasa.

Tathmini ya LHRC ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 katika muswada wa marekebisho hayo ilitambua vifungu vifuatavyo kama tishio kwa uhuru wa kujumuika wa vyama vya siasa: vifungu vinavyofanya shughuli mbalimbali za kisiasa kuwa makosa ya jinai; vifungu vyenye maelezo yenye utata, hivyo kuacha mianya ya kuwa na tafsiri pana na kutumiwa vibaya; vifungu visivyozingatia kanuni za haki asilia; na vifungu vinavyotoa mamlaka makubwa kupita kiasi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

Pia, utafiti uliofanywa na Shirika la Twaweza mwaka 2018 unaonyesha kwamba uelewa wa wananchi kuhusu vyama vidogo vya siasa ni mdogo. Kwa mujibu wa utafiti huo, wananchi

wengi wanavifahamu zaidi vyama vikubwa vitatu vya siasa, ambavyo ni CCM (100%), Chadema (97%) na CUF (83%).

Uelewa mdogo kuhusu vyama vingine unaonyesha haja na umuhimu wa kutoingilia uhuru wa kujumuika na kukusanyika wa vyama vya siasa, ikiwemo kupitia uminywaji wa kukusanyika kisiasa na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yaliyotolewa mwaka 2018.

Mwezi Oktoba 2018, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa Kanuni za Marekebisho ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ambazo zinajumuisha kanuni kadhaa chanya, ikiwemo zinazohakikisha uwazi na uwajibikaji, pamoja na kupambana na rushwa na utakatishaji fedha. Hata hivyo, kanuni hizi pia zinajumuisha kanuni zinazominya ama kutishia uhuru wa mashirika yasiyo ya kiserikali wa kujumuika, ambazo zinayapa mzigo mkubwa mashirika hayo wa kutoa taarifa za mara kwa mara na kuleta ugumu wa utekelezaji wa baadhi ya masharti. Utekelezaji wa kanuni hizi, ambazo zinaacha mianya ya kutumika vibaya, bila kufanyiwa marekebisho kwa kuzingatia maoni ya wanaoguswa nazo kutapelekea kupungua kwa uhuru wa mashirika hayo kufanya kazi zake bila kuingiliwa au kubughudhiwa kinyume na sheria, hivyo kuathiri uhuru wao wa kujumuika.

## 3.3. Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali

Haki ya kushiriki katika utawala au kwenye Serikali inajumuisha haki ya kupiga na kupigiwa kura na haki ya kushiriki katika masuala ya siasa.

Haki ya Kupiga na Kupigiwa Kura: Kwa mwaka 2018, LHRC ilifuatilia matukio kadhaa yaliyopelekea ukiukwaji wa haki ya kupiga na kupigiwa kura wakati wa chaguzi ndogo za marudio zilizofanyika katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara. Matukio makubwa yaliyokuwa nia ya vurugu wakati wa zoezi hilo, ambazo zilipelekea majeraha makubwa kwa baadhi ya wagombea na wanachama wa vyama vya siasa. Wakati wa zoezi hili, vyama vya upinzani vililalamika kuhusiana na ukiukwaji kwa taratibu za uchaguzi, ikiwemo mawakala wao kunyimwa/kucheleweshewa vibali vya kuingia katika vituo vya kupigia kura. Jijini Dar es Salaam, hali hii ilipelekea kutokea kwa maandamano ambayo yalipelekea kuuwawa kwa mwanafunzi wa chuo cha usafirishaji.

Haki ya Kushiriki katika Masuala ya Siasa: Kwa mwaka 2018, uminywaji wa haki za ushiriki, ambazo ni: uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika, uliathiri kwa kiasi kikubwa haki ya kushiriki katika masuala ya siasa na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupungua kwa nafasi ya ushiriki Tanzania Bara.

Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 pia yalichangia kuminywa kwa haki ya kushiki katika masuala ya siasa.

Sheria ya Mapendekezo ya Marebekisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2018 inajumuisha vifungu mbalimbali vinavyominya haki hii, ikiwemo vile ambavyo: vinafanya shughuli mbalimbali za kisiasa kuwa makosa ya jinai; vinavyotoa mamlaka makubwa kupita kiasi kwa Msajili; na vinavyotoa adhabu kali kupita kiasi kwa vyama na wanachama kwa kutozingatia vifungu vya sheria hiyo. Uminywaji huu wa haki za ushiriki umechangia kuendelea kupungua kwa nafasi ya ushiriki nchini Tanzania.

Utafiti kuhusu maoni ya wananchi kuhusu siasa nchini Tanzania, uliofanywa na Shirika la Twaweza mwaka 2018 unaonyesha kwamba Watanzania wengi hawana imani na namna wanavyowakilishwa na wabunge na madiwani wao. Kwa mujibu wa utafiti huo, ni asilimia 44 tu ya wananchi wanaridhia na utendaji kazi wa wabunge wao, huku asiliia 45 wakiridhika na utendaji wa madiwani wao.

SURA YA NNE:
HAKI ZA KIUCHUMI

## Utangulizi

Serikali ya Tanzania ina jukumu la kuhakikisha utekelezaji na ufurahiaji wa haki za kiuchumi kadri ya rasilimali zilizopo chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni, na mikataba mingine ya kimataifa ya haki za binadamu, na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Haki Zilizoangaliwa (2)

Haki ya Kumiliki Mali,
Haki ya Kufanya Kazi

### 4.1. Haki ya Kumiliki Mali

Haki hii imejikita zaidi kwenye ardhi, ambayo inajumuisha kila kitu kilichopo juu yake. Wakati haki ya kumiliki mali ikiendelea kuwa changamoto kwa upande wa wanawake, kwa ujumla utekelezaji na ufurahiaji wa haki hii ulionekana kuimarika kiasi mwaka 2018. Hii ilitokana na hatua mbalimbali za serikali kushughulikia matatizo mbalimbali yanayohusiana na ardhi, ikiwemo migogoro ya ardhi; uzinduzi na utekelezaji wa programu ya usimamizi wa ardhi; na kuimarishwa kwa ulinzi wa haki ya umiliki wa ardhi.




Hata hivyo, migogoro ya ardhi bado iliendelea kuwa changamoto katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara kwa mwaka 2018, hasa migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Kati ya mwezi Julai 2017 na mwezi Machi 2018, jumla ya migogoro ya ardhi 86 kati ya wakulima na wafugaji ilitokea Tanzania Bara, ambapo illipelekea vifo vya watu 44 na kusababisha majeraha kwa watu 75. Ukiacha changamoto ya ufurahiaji wa haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa wakulima na wafugaji, sheria baguzi na ukatili wa kijinsia vilichangia kuminya utekelezaji na ufurahiaji wa haki ya kumiliki na kutumia ardhi kwa upande wa wanawake. Kama inavyoelezewa katika Sura ya Saba ya ripoti hii, ukatili wa kiuchumi ulikuwa miongoni mwa changamoto kubwa zilizowakumba wanawake mwaka 2018.

Pia, gharama za ardhi kuwa kubwa ziliendelea kuleta changamoto kwa wananchi wengi, ambao ni maskini. Masuala mengine yaliyoibuka tena mwaka 2018 ni rushwa na utwaaji ardhi kinyume na sheria unaofanywa na wawekezaji. Wakati wa ziara yake wilayani Bunda, mkoani Mara mwezi ali-yoifanya mwezi Septemba mwaka 2018, Rais wa Tanzania, Mh. John Pombe


Magufuli alitoa onyo kwa wawekezaji wanaotwaa ardhi kwa ajili ya uwekezaji kinyume na sheria. Hii lifuatia malalamiko kutoka kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo kuhusu mwekezaji mmoja ambaye alitwaa ardhi yao bila kuwalipa fidia.

### 4.2. Haki ya Kufanya Kazi

Haki ya kufanya kazi inajumuisha haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi na haki ya mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi iliendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ajira na vijana wengi wanaomaliza elimu ya juu kukosa au kutokuwa na stadi au sifa za kuajiriwa. Kwa mujibu wa tafiti iliyofanywa na Baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki (IUCEA) mwaka 2014, asilimia 61 ya vijana wanaomaliza elimu ya juu hawana stadi au sifa hizo, hivyo kuchangia pia ugumu wao katika kuajiriwa.



Pia, haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi iliendelea kukabiliwa na changamoto nyingine mbalimbali mwaka 2018, ikiwemo: ujira finyu; uminywaji wa uhuru wa kujumuika na makubaliano ya pamoja; mazingira duni ya kufanyia kazi; na uelewa mdogo kuhusu sheria za kazi, haki na wajibu wa mfanyakazi na mwajiri. Mojawapo ya makundi ambayo yaliathirika zaidi na changamoto hizi kwa mwaka 2018 ni walimu. Kwa upande wa wanawake, matukio ya ukatili wa kingono, hususan kuombwa rushwa ya ngono ili kupata kazi au kupandishwa cheo, yaliwafanya wasifurahie vizuri au kikamilifu haki ya kufanya kazi.



Kwa mwaka 2018, haki ya kufanya kazi pia iliathiriwa na kuletwa kwa kikokotoo kipya cha malipo ya pensheni kwa wastaafu, ambacho kilileta mjadala na malalamiko makubwa. Kikokotoo hicho kilielekeza malipo ya asilimia 25 ya mafao kwa mkupuo na asilimia 75 inayobaki kulipwa kama mshahara kila mwezi kwa kipindi cha miaka 12.5 tangu kustaafu. Kabla ya hapo, malipo ya mkupuo yalikuwa asilimia 50 na ya malipo ya kila mwezi nayo asilimia 50. Ilipofika mwezi Disemba 2018, Rais John Magufuli alitoa amri ya kikokotoo hicho kipya kuacha kutumika kwa muda na kurudi katika kikokotoo kilichokuwa kinatumika hapo awali katika kipindi cha mpito.

Pia, wafanyakazi katika sekta za umma na binafsi waliendelea kulalamika kuhusu kodi kubwa ya mshahara (PAYE) na makato ya mkopo wa elimu ya juu. Kodi ya mshahara ni asilimia 30 ya mshahara, huku makato ya mkopo wa elimu

ya juu ni asilimia 15 ya mshahara – ikipanda kutoka asilimia 8 kuanzia mwezi wa Januari mwaka 2017. Kwa mujibu wa ripoti ya Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka wa fedha 2016/2017, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alielezea kwamba jumla ya wafanyakazi 4,830 katika mamlaka za serikali za mitaa 58 walipata mshahara wa chini ya theluthi moja, kinyume na sheria – sababu kubwa ikiwa na kuongezeka kwa makato kutokana na kupanda kwa makato ya mkopo wa elimu ya juu kutoka asilimia 8 hadi 15.


Pia, katika ripoti yake ya mwaka wa fedha 2017/2018, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alibainisha masuala mengine mbalibali yanayoathiri haki ya kufanya kazi, ikiwemo:

Kuwepo kwa madai mbalimbali ya watumishi na malimbikizo ya mishahara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 ambayo hayajalipwa yenye jumla ya Sh.11,141,505,574. Suala hili linashusha mori ya kufanya kazi na kuathiri ufanisi wa utoaji huduma kwa jamii;


Mapungufu katika mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi (OPRAS) wa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

Kuchelewa kuidhinisha upandishwaji vyeo na ongezeko la mishahara kwa watumishi 10,899 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17; na

Upungufu wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao unasababisha mzingo mkubwa kwa watumishi waliopo



Suala jingine kuhusiana na haki ya kufanya kazi liloibua mjadala mwaka 2018 ni ukiukwaji wa haki ya kufanya kazi kwa wafanyakazi wa nyumbani/ndani. Hii ilitokana na ukiukwaji wa haki zao kama wafanyakazi kama vile haki ya kupata mkabata wa ajira; haki ya kulipwa ujira stahiki; haki ya mazingira mazuri ya kazi; na haki ya likizo. Tatiti ya hivi karibuni kuhusu hali ya wafanyakazi wa nyumbani/ndani nchini Tanzania inayonyesha kwamba asilimia 80 ya wafanyakazi hao hawana mikataba ya ajira. Ripoti hiyo pia inaonyesha kwamba wengi wao wanafanyishwa zaidi ya muda uliowekwa kisheria bila kupewa malipo ya ziada; wanalipwa chini ya kiwango kilichowekwa na sheria za kazi Tanzania; hawapewi likizo; hawana taarifa muhimu kuhusu haki zao, na wanatendelwa vibaya na waajiri wao.



SURA YA TANO

# HAKI ZA KIJAMII NA KIUTAMADUNI

## Utangulizi

Haki za kijamii ni pamoja na Haki ya Elimu, Haki ya Afya, Haki ya kupata Maji Safi na Salama, Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa na Haki ya Utamaduni. Haki hizi zinalindwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981, ambayo Tanzania imeridhiria. Haki hizi pia zinapatikana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kama ilivyo kwa haki za kiuchumi, Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki hizi zinafurahiwa na Watanzania kulingana na upatikanaji wa rasilimali. Serikali ina jukumu kubwa la kutengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha kuwa haki hizi zinafurahiwa.

**Haki Zilizoangaliwa (5)**

Haki ya Elimu,
Haki ya Afya,
Haki ya kupata Maji Safi na Salama,
Haki ya Utamaduni
Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa,

### 5.1. Haki ya Elimu



Utekelezaji wa sera ya elimu bila ada umesaidia kuongeza upatikanaji wa elimu ya msingi na sekondari. Hata hivyo, limetokea tatizo ya uhaba mkubwa wa madarasa kwa wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi na kufaulu kujiunga na elimu ya sekondari. Kwa mwaka 2018, uhaba huu uliripotiwa katika mikoa kadhaa ya Tanzania Bara, ikiwemo Shinyanga na Arusha. Changamoto nyingine zilizoathiri upatikanaji na ubora wa elimu kwa mwaka 2018 ni pamoja na: umbali mrefu kati ya nyumbani na shuleni; bajeti isiyotosheleza ya sekta ya elimu; uhaba wa vyoo na matundu ya vyoo; uhaba wa walimu na vifaa vya kujifunzia; mimba za utotoni; ndoa za utotoni; na mazingira duni ya kufanyia kazi ya walimu.

### 5.2. Haki ya Afya



Mwaka 2018, Serikali ilichukua hatua kadhaa kuhakikisha utekelezaji wa haki ya afya Tanzania Bara kulingana na rasilimali zilizopo, ikiwemo maandalizi ya ujenzi wa hospitali za wilaya zaidi ya 60. Hata hivyo, utekelezaji wa haki hii ulendelea kuathiriwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa hospitali, zahanati na vituo vya afya; uhaba wa wafanyakazi katika sekta ya afya; ufinyu wa bajeti; fedha zilizotengwa kwenye bajeti kuchelewa kufika sehemu husika; na uhaba wa vitanda, dawa na vifaa vya afya. Uhaba wa hospitali, zahanati na vituo vya afya uliripotiwa kaitka mikoa kadhaa ya Tanzania Bara, ikiwemo Kigoma, Mwanza (Ukerewe), Tanga (Muheza) na Shinyanga (Kahama). Upatikaji wa huduma za afya kwa gharama nafuu pia uliendelea kuwa changamoto kwa

watu wengi, ikizingatiwa kwamba ni asilimia 30 tu watu wana bima ya afya. Hata hivyo, mwaka 2018 Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mh. Ummy Mwalimu, alieleza kwamba Serikali ina mpango wa kuhakikisha asilimia 50 ya Watanzania wana bima ya afya kufikia mwaka 2020.

### 5.3. Haki ya kupata Maji Safi na Salama

Haki ya kupata maji safi na salama ni haki muhimu ya kiuchumi na kijamii, ambayo inatakiwa kutekelezwa kila siku. Kwa mwaka 2018, kutopatikana kwa urahisi kwa maji safi na salama katika baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara, hasa meaneo ya vijijini, kuliwaathiri sana wanawake na wasichana, ambao walilazimika kutembea umbali mrefu kuchota maji. Mara nyingi wanawake hao wanapochelewa kurudi nyumbani, waume zao huwatuhumu kuwa na wanaume wengine. Kwa wasichana, kutopatikana kwa maji safi na salama kwa urahisi kunawaathiri kwa namna mbalimbali, hasa kusoma shule katika mazingira magumu. Changamoto zinazoikabili haki ya maji safi na salama ni pamoja na: mapungufu katika bajeti; uhaba wa wataalamu katika sekta ya maji; halmashauri kushindwa kufuatilia fedha za miradi ya maji; kushindwa kukamilisha miradi ya maji kwa muda; taasisi za serikali kutolipa bili za maji kwa wakati; kushuka kwa viwango vya maji; sekta binafsi kutowekeza vya kutosha kwenye miradi ya maji; uharibifu wa miundombinu ya maji; upotevu wa maji; na usimamizi usioridhisha wa miradi ya maji.



### 5.4. Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa

Haki ya kuishi katika hali inayofaa inajumuisha haki ya kupata chakula na haki ya makazi yanayofaa. Haki hizi ni haki za muhimu katika kufurahia haki nyingine za binadamu. Haki hizi ni muhimu katika kutekeleza haki nyingine za binadamu. Kwa mwaka 2018, hali ya chakula haikuwa tatizo kubwa. Hata hivyo, matumizi ya vyakula vyenye virutibisho bado ni changamoto, hasa kwa watoto walio maeneo ya vijijini. Kwa upande wa haki ya makazi yanayofaa, bado nyumba nyingi za Watanzania haziko katika hali inayofaa. Kwa watu ambao wakumbwa na adha ya kubolewa nyumba zao mwaka 2017 jijini Dar es Salaam, suala lilileta mtafaruku mkubwa, ufurahiaji wa haki ya kuishi katika hali inayofaa uliendelea kuwa changamoto kwa mwaka 2018.



### 5.5. Haki ya Utamaduni

Haki ya utamaduni ni miongoni kwa haki za msingi za binadamu zinazofurahiwa bila vikwazo nchini Tanzania; na kwa mwaka 2018 hali ya haki hii iliendelea kuimarika. Watanzania, yakiwemo makabila madogo, wapo huru kushiriki katika maisha ya kiutamaduni na kufurahia bidhaa na utambulisho wa kiutamaduni. Serikali iliendelea kukuza Lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, watu wapo huru kuabudu na kutekeleza utamaduni wa kidini.

SURA YA SITA

# HAKI ZA KIUJUMLA

Haki Zilizoangaliwa (2)

Haki ya Maendeleo,
Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili

## Utangulizi

Haki za Kiujumla ni haki ambazo zinafurahiwa na watu wengi. Haki hizi ni pamoja na Haki ya Maendeleo na Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili.

### 6.1. Haki ya Maendeleo

Haki hii inajumuisha ushiriki katika kuchangia na kufurahia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Kwa mwaka 2018, maendeleo ya kisiasa yalizorota, sababu kubwa ikiwa ni uminywaji wa haki za ushiriki, ambao ulipelekea ushiriki mdogo wa watu katika maendeleo ya kisiasa. Haki za ushiriki kama vile uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika ziliathiriwa na vitendo hatua mbalimbali zilizochukuliwa, ikiwemo utungaji wa sheria na kanuni ambazo zinaminya haki hizo.

Maendeleo ya kijamii yanategemea utekelezaji na ufurahiaji wa haki za kijamii kama vile haki ya elimu, haki ya afya, haki ya maji safi na salama na haki ya kuishi katika hali inayofaa. Kwa upande wa elimu, utekelezaji wa sera ya elimu bila ada ulisaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza upatikanaji wa elimu msingi na mamlaka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara zimeendelea kusimamia utekelezaji wake, ikiwemo kuhakikisha wazazi wanawapeleka watoto shule. Hata hivyo, zoezi hili limekuja na changamoto ya uhaba wa madarasa kuwawezesha wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa mwisho wa elimu ya msingi kuendelea na elimu ya sekondari. Ukusanyaji kodi ni muhimu sana kwa ajili ya kutekeleza haki za kijamii, ili kuiwezesha Serikali kutoa huduma za kijamii kama vile chakula, maji, makazi na afya, hasa kwa kaya maskini. Hivyo basi, ukwepaji wa kodi katika sekta mbalimbali kwa mwaka 2018 pia ulitishia utekelezaji wa aki za kijamii na kiuchumi.

Pamoja na juhudi na hatua mbalimbali ambazo Tanzania imepiga katika maendeleo ya kiuchumi, changamoto kubwa bado ni namna gani maendeleo hayo yanapunguza umaskini ili kuleta maendeleo ya kibinadamu. Bado watu wengi nchini ni maskini, wakiishi chini au juu kidogo ya Dola moja ya Kimarekani.

Uwepo wa bidhaa feki na zilizo chini ya viwango pia uliathiri ufurahiaji wa haki ya maendeleo pamoja na haki nyingine za binadamu, pamoja na haki za walaji mwaka 2018. Ripoti ya mwaka 2017 kuhusu hali ya bidhaa feki nchini Tanzania ya Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) inaonyesha kwamba bidhaa feki zinaisababishia serikali upotevu wa kodi yenye thamani ya takribani Dola milioni 4 za Kimarekani kila mwaka. Uwepo wa bidhaa feki na zilizo chini ya kiwango pia unasababisha kupotea kwa ajira; unaathiri afya; unasababisha wateja wasiamini bidhaa za kampuni fulani; kusababisha makampuni kupeteza hisa katika masoko; na kuhatarisha usalama.

## 6.2. Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili

Mambo makuu yaliyokuwa tishio kwa utekelezaji wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili kwa mwaka 2018 ni pamoja na: rushwa kwenye sekta ya madini; utwaaji ardhi bila kufuata utaratibu; ukwepaji kodi; na baadhi ya maeneo kukosa rasimali ya maji safi na salama. Kwa mfano, mwaka 2018 maafisa kadhaa kutoka Mgodi wa Dhahabu wa North Mara pamoja na watendaji kadhaa wa serikali katika Mkoa wa Mara walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa tuhuma za makosa ya kutoa na kupokea rushwa tangu mwaka 2006 ili kuupa mgodi huo upendeleo wakati wa tathmini na kuminya haki za wakazi wa eneo la karibu na mgodi.



**SURA YA SABA**

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

## Utangulizi

Haki za msingi za makundi maalum ambazo huwa zinavunjwa mara nyingi ni Haki dhidi ya Ukatili, Haki ya Usawa na Kutobaguliwa, na Haki ya Kupata Huduma Bora za Kijamii.

| Makundi yaliyoangaliwa |
| --- |
| Wanawake, Watoto,<br>Watu wenye Ulemavu,<br>Wazee,<br>Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |

### 6.1. Haki za Wanawake

Ukiacha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki za wanawake kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni ya haki za wanawake pekee. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol). Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni ubaguzi dhidi ya wanawake unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu. Mwaka 2018, wanawake waliendelea kubaguliwa na kufanyiwa ukatili, hali iliyoathiri ufurahiaji wa haki zao za kuishi, kumiliki mali na usawa.

**Masuala makuu yaliyoathiri haki za wanawake mwaka 2018**

- Ukatili wa kiuchumi
- Ukatili wa kimwili na kisaikolojia
- Ukatili wa kingono
- Ulawiti kwenye ndoa
- Rushwa ya ngono – ambayo ilikuwa changamoto kwa wanawake, ikiwemo wanafunzi wa kike vyuoni
- Manyanyaso katika utoaji wa matunzo ya mtoto, ambapo baba anamlazimisha mama kulala naye ndipo atoe matunzo



Kwa mwaka 2018, matukio mbalimbali ya ukatili, yakiwemo ya ukatili wa kimwili, kiuchumi na kingono – ikiwemo vipigo, ubakaji, utelekezaji, utumikishwaji na ulawiti katika ndoa – yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara. Katika vyombo vya habari, matukio ya ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake yaliripotiwa zaidi mwaka 2018 ukilinganisha na mwaka 2017. Matukio hayo ni pamoja na tukio lilitokea mkoani Dodoma, ambapo mwanaume mmoja alikamatwa na polisi kwa kumchoma hadi kufa mke wake – ambaye alikuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dodoma; pamoja na tukio

la mwanaume mmoja Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani, kumpiga mke wake – ambaye alikuwa nesi – na kitu kizito kichwani na kumuua.

Kwa upande wa ukatili wa kingono, takwimu za polisi za uhalifu wa ubakaji zinaonyesha katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Juni mwaka 2018, jumla ya matukio 1,218 ya ubakaji wa wanawake yaliripotiwa. Katika mikoa takribani nusu ambayo LHRC iliitembelea mwaka 2018, ukatili wa kingono ulionekana kuwa mojawapo ya aina kuu za ukatili dhidi ya wanawake unaotokea katika maeneo hayo. Mikoa hii ni Songea, Tabora, Mbeya, Singida na Kilimanjaro. Mojawapo ya vitendo vya ukatili wa kingono vilivyoripotiwa sana mwaka 2018 ni wanawake kulazimishwa na wenza wao kufanya mapenzi kinyume na maumbile.

Kwa kushirikiana na Shirika la Twaweza, LHRC ilifanya uchunguzi mdogo mkoani Kigoma kufuatia kupokea taarifa za kushtusha za matukio ya ubakaji wa wanawake mkoani humo unaofanywa na kikundi cha vijana wanaojiita TELEZA, ambao huwavamia wanawake nyumbani usiku wakiwa na silaha na kuwabaka. LHRC na Twaweza waliweza kukusanya taarifa mbalimbali za matukio hayo ya tangu mwaka 2017. Matukio hayo yanajumuisha: ubakaji wa mwanamke ambaye alikuwa amerudi nyumbani kutoka kuchota maji usiku mwaka 2017; tukio la mwaka 2017 la ubakaji wa bibi wa miaka 60, baada ya kupigwa na chuma kichwani; tukio la ubakaji wa mwanamke mwenye miaka 36, ambaye alidai kubakwa mara 6 kuanzia mwaka 2017 hadi mwanzoni mwa 2019, jambo lililopolekea aamue kununua silaha ili ajilinde dhidi ya wabakaji hao; ubakaji wa mwanamke alikuwa na mimba ya miezi 8 mwaka 2018; na ubakaji wa wazee wawili, mmoja akiwa na miaka 70. Matukio ya ubakaji na mauaji ya wanawake mwaka 2018 pia yaliropotiwa wilayani Monduli mkoani Arusha. LHRC inalaani matukio haya ya ukatili dhidi ya wanawake na kuziomba mamlaka husika, ikiwemo Jeshi la Polisi, kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha wanaofanya vitendo hivi vya kinyama wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.



Rushwa ya ngono ilionekana pia kuwa changamoto kubwa kwa wanawake mwaka 2018, hasa wanawake vijana wanaotafuta kazi. Taarifa za wanawake wanaoshurutishwa kufanya mapenzi na waajiri ili kupata kazi au kupandishwa cheo zimeendelea kuwa nyingi. Hali hii imekuwa ikiwa katisha tamaa wanawake vijana katika kufatufa ajira. Mwezi wa Novemba 2018, mhadhiri mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Vincensia Shule, alivunja ukimya kuhusu suala hili na kuandika kuhusu kukithiri kwa vitendo vya rushwa ya ngono katika chuo hicho kwenye ukarasa wake wa Twitter muda mfupi baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. John Pombe Magufuli kutembelea chuo hicho na kuzindua maktaba mpya ya kisasa.

Tathmini iliyofanywa na LHRC ilionyesha kwamba ukatili wa kiuchumi ulikuwa ndio aina ya ukatili dhidi wa wanawake uliotamalaki zaidi katika mikoa sita kati ya kumi ambayo ilitembelea. Mikoa hii ni Mbeya, Iringa, Shinyanga, Singida, Ruvuma na Kilimanjaro. Mkoani Ruvuma, ukatili wa kiuchumi ulionekana kuwa changamoto zaidi katika Wilaya ya Namtumbo.


Sababu zinazochangia ukatili dhidi ya wanawake ni pamoja na: imani za kishirikina, wivu na visasi; ulipaji mahari; uelewa mdogo kuhusu sheria; ulevi miongoni mwa wanaume; elimu ndogo; na mila na tamaduni zenye madhara.

Suala jingine ambalo liliathiri haki za wanawake mwaka 2018, hususan haki za uzazi, ni ushauri uliotolewa na Rasi kwa wanawake, akiwaasa kuachana na uzazi wa mpango na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kusimamisha urushaji wa matangazo ya uzazi wa mpango kwenye redio na televisheni mwezi Septemba mwaka 2018.

## 6.2 Haki za Watoto

**Kanuni kuu nne za ulinzi wa mtoto**

- Kutobaguliwa
- Kuzingatia maslahi bora ya mtoto
- Haki ya kuishi, kukua na kuendelea
- Kuheshimu maoni ya mtoto




Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa kufikia katikati ya 2017 na katikati ya 2018

**Chanzo:** Takwimu za Matukio ya Uhalifu za Jeshi la Polisi, 2017 & 2018


Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maamuzi yoyote kuhusu mtoto kanuni ya maslahi bora ya mtoto lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi. Hata hivyo, watoto wameendelea kuwa wahanga wa aina mbalimbali za ukatili, hasa ukatili wa kingono (ubakaji na ulawiti).



## Ukatili wa Kingono:

**Dondoo Muhimu**

- Matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto kuongeza kwa kiasi kikubwa
- Ukatili wa kingono unawaweka watoto katika hatari ya kuambukizwa UKIMWI
- Ukatili wa kingono dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenzao: Mara nyingi watoto wakubwa huwafanyia wadogo, hasa shuleni na nyumbani
- Imani za kishirikina miongoni mwa sababu za kukithiri kwa ukatili wa kingono dhidi ya watoto
- Umbail mrefu kufika shuleni unachangia ukatili dhidi wa watoto, hasa ukatili wa kingono
- Hatua chanya: Serikali kuanzisha madawati ya jinsia mashuleni – haya yatasaidia katika juhudi za kupambana na ukatili dhidi ya watoto
- Majirani, ndugu wa karibu, madereva bodaboda na walimu, miongoni mwa wafanyaji wa ukatili wa kingono dhidi ya watoto
- Malalamiko kuhusu kuongezeka kwa makosa ya kingono dhidi ya watoto katika wilaya mbalimbali za Tanzania Bara
- Juhudi za Mhimili wa Mahakama katika kupambana na ukatili wa kingono dhidi ya watoto




Kwa mwaka 2018, uhuru dhidi ya ukatili ulionekana kuwa haki iliyokiukwa zaidi Tanzania Bara, sababu kubwa ikiwa ukatili dhidi ya watoto. Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliongezeka kutoka 4,728 kufikia katikati ya mwaka 2017 hadi matukio 6,376 kufikia katikati ya mwaka 2019. Changamoto kubwa kwa watoto ilikuwa ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti. Aina hii ya ukatili ilitajwa kama changamoto kubwa kwa watoto katika wilaya zote 20 za mikoa 10 ambazo LHRC ilizitembelea mwaka 2018. Katika sehemu nyingi zilizotembelewa, ukatili wa kingono dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenyewe ulitajwa kuwepo na kuongezeka, hasa mashuleni. Matukio ya ubakaji wa watoto yaliongezeka kutoka 759 katika kipindi cha miezi sita mwanzo ya mwaka 2017 hadi kufikia matukio 2,365 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Taarifa kuhusu matukio ya haki za binadamu yaliyoripotiwa na vyombo vya habari mwaka 2018 zilizokusanywa na LHRC zinaonyesha kwamba asilimia 91 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa na vyombo hivyo yalikuwa ni ya ukatili wa kingono, huku asilimia 9 yakiwa ni ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia. Taarifa mbalimbali za kuongezeka kwa uhalifu wa kingono dhidi ya watoto pia zilitolewa katika maeneo mbalimbali za Tanzania Bara, kama vile Mpwapwa-Dodoma, Chunya-Mbeya, Misungwi-Mwanza, Hai-Kilimanjaro na Tarime-Mara.

Majirani na ndugu wa karibu waliendelea kutajwa kama watendaji wakuu wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Hata hivyo, madereva bodaboda na walimu pia walitajwa kushiriki katika vitendo mbalimbali vya ukatili wa kingono dhidi ya watoto mwaka 2018.

Mambo yanayochangia kushamiri kwa ukatili dhidi ya watoto Tanzania Bara ni pamoja na: watoto kukosa malezi na uangalizi bora; uelewa mdogo kuhusu malezi miongoni mwa wazazi na walezi; umaskini, ambao huwaweka hatarini zaidi wasichana kushawishiwa na wanaume; watoto kuachwa na wazazi peke yao kwa muda mrefu au kuachwa kuishi na mzazi mmoja kwa kipindi kirefu; ulevi miongoni mwa wanaume; tabia ya wazazi kupendelea kumaliza kesi za ukatili dhidi ya watoto kupitia 'kikao cha familia' ili 'kuficha aibu ya familia.' Mambo mengine ni: wanaume kuwatelekeza wake zao na watoto na kwenda kuoa au kuishi na wanawake wengine (dogodogo); mazingira duni ya shule na umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni – hivyo kuwafanya wasichana kuwa hatarini kushawishiwa na madereva bodaboda; udadisi, hasa kwa upande wa ukatili wa kingono dhidi ya watoto unaofanywa na watoto wenzao; na wazazi kutotenga muda wa kutosha kukaa na watoto wao na kujua matatizo yao.

Ukatili wa kingono dhidi ya watoto, hasa wasichana na wanawake vijana, unawaweka katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Hii itaathiri juhudi za Tanzania za malengo ya 90-90-90 ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Kuna kesi ya mama anafanya biashara ya pombe. Akirudi anakuja na hawala wamelewa. Yule bwana akimaliza kufanya mapenzi na mama anamgeukia binti (wanalala chumba kimoja), ambaye ni mtoto wa miaka 13. Wanakuja wanaume tofauti mara kwa mara na wakati mwingine wanaume wanarudi mchana na kumuingilia tena mtoto. Bahati nzuri mtoto aliokolewa na maafisa ustawi na hakukutwa na maambukizi ya VVU.

Afisa Ustawi, Singida (Manispaa)

Umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shule unachangia pia vitendo vya ukatili, kwa kuwa baadhi ya wasichana wanabakwa wakati wakienda au kutoka shule. Mfano, kuna mtoto wa miaka 9 alikuwa na wenzake wametoka shule, akavutwa kichakani, akabwa na kulawitiwa. Mwenzie akakimbia kwenda kutoa taarifa. Tukio hili lilitokea mwezi wa 4 mwaka 2018 katika Kijiji cha Uvanga, Kata ya Iksimani.

Afisa Ustawi, Iringa (Halmashauri ya Wilaya)

Imani za kishirikina pia ni sababu kubwa za ukatili kwa watoto. Mategemeo ya kupata pesa nyingi yanasababisha ukatili hasa ubakaji kwa watoto wa kike.

Kitengo cha Ustawi wa Jamii, Mbeya

Mtoto mmoja ambaye alikuwa amemaliza form 4 alivyorudi nyumbani akawa anamfanyia mdogo wake. Anamshikia panga kumtishia akikataa.

**Kitengo cha Ustawi wa Jamii, Moshi (Manispaa)**

Taarifa zimekuwa zikipokelewa kutoka mashuleni kuhusiana na masuala ya ulawiti wa watoto. Wakiamua kufuatilia walimu wanaogopa kutoa taarifa na kuogopa kuchafua sifa ya shule zao, hasa shule binafsi.

**Kitengo cha Ustawi wa Jamii, Mbeya**

Kuna mtoto wa kiume wa miaka 6 alikuwa boarding school, alikuwa anafanyiwa ukatili shuleni.

Baada ya wazazi kuona hali ya kiafya inazidi kudhoofu wakampeleka hospitali kumpima na kugundulika kuwa ni HIV positive, ugonjwa aliopata sababu ya kulawitiwa wakati yuko shuleni. Baba mzazi alishtuka, akapata stroke, akafa.

**Kitengo cha Ustawi wa Jamii, Tabora (Manispaa)**

Mtoto mmoja alikuwa HIV positive, ila alikuwa analawitiwa na mtu mzima, ambaye naye alikuwa anamlawiti pia mtoto mwingine. Mtoto akazoea na yeye akaanza kuwafanyia hivyo watoto wengine.

**Kitengo cha Ustawi wa Jamii, Tabora (Manispaa**


Kesi nyingi katika mahakama ya watoto ni za ulawiti na ubakaji. Baadhi ya watoto huwa pia wanashiriki katika gang-rape. Kuna mtoto wa miaka 7 alimlawiti mtoto wa miaka 5. Pia kuna mtoto wa miaka 12 ambaye ana kesi mbili tofauti za ulawiti.

**Afisa Ustawi wa Jamii, Moshi (Manispaa)**

Katika tukio moja, lililotokea mwezi wa 7 mwaka 2018, mtoto mmoja mwenye miaka 11 alibakwa na baba yake mzazi kwa muda mrefu. Mtoto huyo alikuwa akiishi na mama yake baada ya kutengena na baba yake. Alikuwa anaenda kwa baba yake kuchukua mahitaji, ila kila akienda anabakwa. Hatimaye ameambukizwa HIV. Kesi ipo mahakamani.

**Afisa Ustawi wa Jamii, Mbeya (Halmashauri Jiji)**

Ukatili wa Kimwili na Kisaikolojia: LHRC iliweza kukusanya jumla ya matukio 13 ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya watoto kupitia uchambuzi wa matukio yaliyoripotiwa na vyombo vya habari. Matukio mengine mengi yaliripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi, kupitia madawati ya jinsia na watoto. Mojawapo ya matukio ya ukatili wa kimwili dhidi ya watoto yaliyolishtua taifa ni kuchapwa na kupigwa kwa mtoto wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Kibeta wilayani Bukoba mkoani Kagera, Sperious Eradius, na mwalimu wake, Respicious Patrick (anayejulikana pia kama Mtazangira), hadi kupelekea kifo chake. Tukio hili lilitokea mwezi wa nane mwaka 2018 shuleni hapo. Tukio jingine, ambalo LHRC ilienda kulifuatilia, lilitokea mkoani Morogoro, ambapo mtoto mwingine mwenye miaka 10, mwanafunzi wa shule moja ya msingi wilayani Kilosa, alichapwa vibaya na walimu wake, hadi kupelekea kulazwa katika Hospitali ya Muhimbili jijini Dar es Salaam.



Ndoa za utotoni na mimba za utotoni: Mimba za utotoni na ndoa za utotoni ziliendelea kukwamisha utekelezaji na ufurahiaji wa haki za watoto, husasan wasichana, mwaka 2018. Taarifa mbalimbali za ndoa za utotoni ziliripotiwa mwaka 2018, ikiwemo katika maeneo ya Nkasi-Rukwa, Same-Kilimanjaro, and Serengeti-Mara. Pia, ndoa hizi ziliendelea kuwa changamoto katika mikoa kama Tabora na Shinyanga. Visababishi vya ndoa za utotoni ni pamoja na mahari, uhaba wa shule za sekondari, kushurutishwa na wazazi na ukeketaji.

Mwaka 2018, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mh. Aggrey Mwanri, na timu yake walifanya jitihada kadhaa za kushughulikia tatizo la ukatili dhidi ya watoto na ndoa za utotoni zilizokithiri mkoani humo, pamoja na kukuza haki ya elimu kwa wasichana. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wanajamii na kuhakikisha sheria inafuata mkondo wake pale ambapo vitendo hivyo vinavyominya haki za wasichana vinapotokea.



Mimba za utotoni pia zilikuwa mojawapo ya changamoto kubwa kwa watoto wa kike mwaka 2018, ambapo LHRC iliweza kukusanya matukio ya mimba za utotoni zaidi ya 1000 yaliyoripotiwa katika mikoa takribani 10 ya Tanzania Bara. Ongezeko la mimba za utotoni linamaanisha kwamba wasichana wengi wanashiriki ngono isiyo salama, hivyo kuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Suala hili lisiposhughulikiwa litaathiri juhudi za Serikali za kutokomeza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI miongoni mwa wasichana na wanawake vijana.

Ubaguzi dhidi ya watoto: Ubaguzi dhidi ya watoto uliendelea kuwa changamoto kubwa kwa watoto wa mtaani na watoto wenye ulemavu mwaka 2018. Watoto hawa walikumbwa na changamoto ya kubaguliwa na kunyanyapaliwa. Hali hii huwapelekea kutofurahia kikamilifu

haki zao za msingi kama binadamu sawa na watoto wengine, kama zilizovyoainishwa kwenye sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto.

Mara kwa mara, watoto wa mtaani waliopo kwenye miji na majiji mbalimbali nchini Tanzania hufanyiwa bughudha na mamlaka pamoja na wanajamii, wakinyimwa kufurahia haki zao za msingi kama vile uhuru wa kujumuika na uhuru wa kukusanyika. Wamekuwa pia wakizuiwa kukusanyika na kutumia maeneo ya umma na kukamatwa kiholela kila mara. Watoto wa mtaani wapo katika hatari zaidi ya kufanyiwa unyanyasaji na ukatili. Kwa kutambua hatari hii na kukua kwa tatizo la kutoheshimu haki za watoto wa mtaani, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto ilitoa Maoni ya Jumla Na. 21 ya mwaka 2017 kuhusu Watoto walio katika Mazingira ya Mtaani, yanayozikumbusha Serikali za nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu majukumu yake ya kulinda na kuheshimu haki za watoto wa mtaani chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989.



Mwezi Mei 2018 ilitolewa ripoti kuhusu watoto wa mtaani kufuatia utafiti uliofanyika mwaka 2017. Ripoti hii inaelezea idadi ya watoto hao wakati wa mchana na wakati wa usiku katika maeneo ya mtaani. Ufafiti ulifanyika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya na Mwanza. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kwamba kuna jumla ya watoto wa mtaani 6,393 wakati wa mchana kwenye majiji haya, ambapo asilimia 76 ni wa kiume na asilimia 24 ni wa kike, huku usiku wakiwa ni 1,385 (asilimia 70 wa kiume, asilimia 30 wa kike). Matokeo yanaonyesha pia kwamba kunakuwa na ongezeko kubwa la watoto wa kike wakati wa usiku kwa kuwa wanajihusisha na biashara ya ngono. Asilimia 86 wa watoto wa kike wanaoishi na kufanya kazi mitaani waliohesabiwa usiku walikuwa wanajihusisha kwenye biashara hiyo, suala ambalo linawaweza katika hatari ya kufanyiwa ukatili. Asilimia 44 ya watoto hao walikuwa na miaka kati ya 11 – 14. Idadi kubwa ya watoto hao wa kike wanaojihusisha na biashara ya ngono usiku ilikuwa Iringa (33%) na ndogo ikiwa ni Dar es Salaam (9%).

Watoto wenye ulemavu pia waliendelea kufanyiwa ubaguzi katika ngazi za familia na jamii, ikiwemo kubaguliwa na wazazi wao wenyewe. Taarifa za baadhi ya wazazi 'kuwaficha' watoto wao wenye ulemavu ndani, na wakati mwingine kuwanyima fursa ya kupata elimu sababu ya ulemavu ziliripotiwa katika mikoa kumi ya Tanzania Bara ambayo LHRC iliitembelea mwaka 2018. Pia, kwa wale wanaofanikiwa kupata fursa ya elimu, kwa mwaka 2018 waliendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali katika kufurahia haki ya elimu, ikiwemo uhaba wa miundombinu na vifaa vya kujifunzia.

## 6.3. Haki za Watu wenye Ulemavu


Kuna mkataba maalum wa kimataifa unaolinda haki za watu wenye ulemavu, uitwao Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD). Haki hizo ni pamoja na haki ya usawa na kutobaguliwa, haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na usalama wa mtu, haki ya kutoteswa, haki dhidi ya ukatili, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya kufanya kazi na kuajiriwa.

Mkataba huu umeridhiwa na Tanzania na kutungiwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Watu wenye ulemavu wanahitaji huduma maalum zitakazowawezesha kufurahia haki za binadamu sawa na watu wengine.

Kwa mwaka 2018, LHRC iliangazia changamoto mbalimbali zinazowakumbwa watu wenye ulemavu, ambazo zinawafanya washindwe kufurahia kikamilifu haki za usawa na kutogabuliwa. Changamoto hizo ni pamoja na: ufinyu wa bajeti ya kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu; umaskini wa kipato; kukosekana miundombinu rafiki; uhaba wa vifaa vya kujifunzia shuleni kwa watoto wenye ulemavu (hivyo kupelekea elimu kutokuwa jumuishi); uhaba/ukosefu wa ajira; na unyanyapaa.

## 6.4. Haki za Wazee


Tofauti na makundi mengine, hakuna mkataba maalum wa kulinda na kusimamia haki za wazee. Hata hivyo, kama binadamu wengine, wazee wana haki mbambali za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Mikataba hiyo ni pamja na Mkataba Nyongeza kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika (Mkataba wa Maputo); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICESCR); na Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD).



Kwa mwaka 2018, ukatili uliendelea kuwa changamoto kubwa kwa wazee Tanzania Bara. Aina ya ukatili ambayo wazee hao walikumbana nazo ni pamoja na ukatili wa kimwili unaosababishwa na imani za kishirikina. Kama ilivyojadiliwa katika Sura ya Pili ya ripoti hii, LHRC ilikusanya matukio yapatayo matatu ya mauaji ya wazee sababu ya imani za kishirikina. Matukio haya ni: kuuwawa kwa mzee kwenye miaka 65 wilaya ya Kaliua mkoani Tabora;

mzee wa miaka 77 kuuwawa kikatili na watu sita, wakiwemo wanawe, Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro; na mauaji ya kikongwe wa miaka 70 wilayani Ileje mkoani Songwe.

Akisoma hotuba ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani, Mh. Dkt. Mwigulu Nchemba (MB), alisema kwamba kuanzia mwezi Julai 2017 hadi mwezi Machi 2018, jumla ya matukio 117 ya mauaji ya wazee yaliripotiwa Tanzania Bara (91 wanaume, 26 wanawake). Mkoa wa Tabora uliongoza kwa mauji haya (25), ukifuatiwa na mikoa ya Songwe (12), Kagera (10) na Rukwa (10).




**#Mauaji ya wazee katika mikoa 13 ya Tanzania Bara, kuanzia mwezi Julai 2017 hadi mwezi Machi 2018**

Chanzo: Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, 2018/2019



## 6.5. Haki za Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wana haki na wajibu mbalimbali kama inavyoainishwa kwenye Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008, ikiwemo haki ya kutobaguliwa, haki ya kupata huduma za afya na wajibu wa kutoambukiza wengine ukimwi kwa makusudi. Sheria ya UKIMWI inakataza ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na hili ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi Milioni 2 au kifungo kisichozidi mwaka 1 au vyote.

Kwa mwaka 2018, LHRC haikupata malalamiko yoyote ya ubaguzi dhi-di ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, unyanyapaa umeendelea kuwa changamoto kubwa kwa watu hawa na kuwafanya washindwe kufurahia na kutekeleza na kufurahia baadhi ya haki zao za binadamu kikamilifu.

SURA YA NANE

# RUSHWA, UTAWALA BORA NA HAKI ZA BINADAMU

Rushwa huathiri uwezo wa Serikali kusimamia na kuhakikisha haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zinafurahiwa kulingana na uwepo wa rasilimali. Matumizi mabaya ya mali za umma yanapunguza nguvu ya Serikali kuweza kutoa huduma za kijamii kama maji, elimu na afya kwa wananchi, hivyo kuathiri haki za maji, elimu na afya. Haki za kiraia na kisiasa kama vile haki ya kuishi, upatikanaji haki, haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa haki pia zinaathiriwa na rushwa.

Rushwa katika mfumo wa haki hutengeneza maafisa polisi, wachunguzi, mahakimu na majaji ambao ni wala rushwa na husababisha kutokuwepo usawa mbele ya sheria na kutosikilizwa kwa haki. Rushwa wakati wa uchaguzi inaweza kuwakatisha watu tamaa kufurahia haki zao za kisiasa, kama vile haki ya kupiga kura.

Tafiti za hivi karibuni kuhusu rushwa nchini Tanzania zilizofanywa na mashirika kama Twaweza, REPOA na Transparency International zinazonyesha watu wengi kuwa na mtazamo wa kupungua kwa rushwa nchini Tanzania. Hali hii inaweza kuwa inatokana na kuongezeka kwa juhudi za kupambana na kuminya mianya ya rushwa chini ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli, ukilinganisha na uongozi uliopita. Kwa mujibu wa ripoti ya mitazamo kuhusu rushwa ya shirika la Transparency International ya mwaka 2018, Tanzania iliendelea kupata pointi 36, ikiwa ni pointi 4 zaidi ya ilizopata kwa mwaka 2016. Hata hivyo, rushwa bado ni tatizo kubwa katika sekta mbalimbali, hivyo juhudi zaidi zinahitajika kupambana na tatizo hili. Mapambano dhidi ya rushwa yangefanikiwa zaidi iwapo sheria mpya mbalimbali ambazo zimetungwa kuanzia mwaka 2015 zisingeminya haki ya uhuru wa kujieleza.

Kwa mwaka 2018, kashfa kubwa ya rushwa ilikuwa ni ile inayoihusisha Mgodi wa Dhahabu wa North Mara, ambapo maafisa kadhaa wa mgodi huo walifikishwa mahakamani kwa makosa ya kutoa rushwa kwa watendaji/maafisa wa serikali ili kupata upendeleo wakati wa upimaji wa ardhi kwa ajili ya kupanua eneo la mgodi huo na kupelekea kuminya na kukiuka haki zinazohusiana na ardhi za wakazi wa maeneo ya mgodi huo.

Mwaka 2018 pia ulikiwa mwaka ambao vitendo vya rushwa ya ngono vilianikwa na wadau mbambali. Mwezi Novemba 2018, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Vincesia Shule, aliandika katika akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa Twitter kuhusu rushwa ya ngono katika chuo hicho, akimuomba Rais aingilie kati, muda mfupi baada ya Mh. Rais John Pombe Magufuli kutembelea chuo hicho.

Katika twiti yake, mhadhiri huyo alieleza kwamba rushwa ya ngono imekithiri katika chuo hicho. Pia, tafiti iliyofanywa na shirika la Internews mwaka 2018 ilionyesha kwamba kukithiri kwa rushwa ya ngono vyuoni na mahala pa kazi nchini Tanzania. Mwezi Disemba 2018, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mh. Richard Kasesela, pia alilamika kuhusu tatizo la rushwa ya ngono kukua katika wilaya yake.

Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali ilioyesha dalili za rushwa kwenye miradi mbalimbali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Ripoti hiyo pia imeonyesha matumizi ya fedha kinyume na taratibu katika mamlaka mbalibali za serikali za mitaa.

SURA YA TISA

# MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

## Utangulizi

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha sheria zinazolinda haki za binadamu na taasisi mbalimbali ambazo zina jukumu la kusimamia sheria hizo na kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Kuna mifumo ya kataifa, mifumo ya kikanda na mifumo ya kimataifa.

## 9.1 Mifumo ya Kitaifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha taasisi muhimu kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Mahakama na Vyombo vya Dola kama vile Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Vyombo hivi vipo kwa mujibu wa sheria.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora: Tume hii ilianzishwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na jukumu lake kubwa ni kuimarisha na kulinda haki za binadamu, ikihakikisha zinaheshimiwa, na kusimamia utawala bora. Pia, Tume huishauri Serikali na taasisi zake kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora na hupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu toka kwa wananchi na kuyafanyia kazi.

Mahakama: Mahakama ni chombo muhimu sana katika ulinzi wa haki za binadamu, ambacho hutoa tafsiri mbalimbali za sheria zinazohusu haki za binadamu, husikiliza kesi na kutoa maamuzi na nafuu za kisheria. Mhimili huu ni muhimu na hutakiwa kuwa huru katika kuchunga mienendo na matendo ya mihimili mingine, ambayo ni Serikali na Bunge.

Vyombo vya dola: Hivi ni pamoja na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, ambavyo vina nafasi na jukumu kubwa la kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Jeshi la Polisi lina jukumu la kusaidia watu kufikia haki kwa kufanya uchunguzi na kuwafikisha watuhumiwa au wavunjifu wa haki za binadamu mahakamani. Magereza huwalinda wanajamii dhidi ya watu waliohukumiwa kutumikia vifungo kwa kufanya uhalifu ambao unahatarisha haki za binadamu, na hivyo uwepo wake huimarisha ulinzi wa haki za binadamu.

### Changamoto zinazoikumba mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu

- Rushwa Ucheleweshaji katika uchunguzi na uendeshaji wa kesi
- Mazingira duni ya kufanyia kazi kutokana na uhaba wa vifaa vya kazi
- Msongamano wa wafungwa
- Ufinyu wa bajeti
- Uelewa mdogo kuhusu haki za binadamu, ikiwemo haki za mtuhumiwa

## 9.2. Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya kikanda na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu, ambayo inaunda vyombo mbalimbali vya kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo na nchi wanachama.

Chini ya Umoja wa Mataifa kuna mfumo wa kutathmini haki za binadamu uitwao Mpango wa Kimataifa wa Kujitathmini juu ya Masuala ya Haki za Binadamu (UPR) au Tathmini ya Haki za Binada-

mu ya Umoja wa Mataifa, ambao unasimamiwa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Mfumo huu unalenga kuboresha hali ya haki za binadamu katika nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa. Nchi wanachama, ikiwemo Tanzania, huwasilisha ripoti kila baada ya miaka 5 ikielezea ni hatua gani imechukua kuboresha haki za binadamu kulingana na wajibu ulioanishwa katika mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo zimeridhia. Mara ya mwisho Tanzania kushiriki katika mchakato huu ni mwaka 2016, ambapo Serikali ilipeleka ripoti yake ya utekelezaji wa haki za binadamu na mashirika yasiyo ya kiserikali kupeleka ripoti mbadala.

Ukiacha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, vyombo vingine katika ngazi za bara na kimataifa zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yanayohusiana na haki za binadamu katika mikataba iliyoridhiwa ni pamoja na Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (HRC), Kamati ya Haki za Mtoto (CRC), Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (CESCR), Kamati ya Kuondoa aina Zozote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Kamati ya Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) na Kamati ya Wataalamu katika Masuala ya Haki na Ustawi wa Mtoto Afrika (ACERWC). Tanzania ina wajibu wa kutoa taarifa za haki za binadamu kwa vyombo hivi kila baada ya muda fulani. Hata hivyo, siyo mara zote ripoti hizo zimekuwa zikitumwa au kutumwa kwa wakati. Pia, kwa upande wa Afrika kuna Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambayo ipo Arusha, Tanzania) na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambapo nchi wanachama wa Umoja wa Afrika hutakiwa kutuma ripoti na pia hupokea na kusikiliza malalamiko kuhusu haki za binadamu).

Kuna taratibu za kupekeleka malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu endapo mhanga wa ukiuwaji huo hajaridhika na nafuu aliyopata katika mifumo ya kitaifa ya utoaji haki.

Pamoja na kuwepo kwa mifumo mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania inaweza kuitumia, matumizi ya mifumo hii ya mtu mmoja mmoja, wanasheria na asasi za kiraia yameendelea kuwa madogo.

SURA YA KUMI

# MASUALA MENGINE YANAYOATHIRI HAKI ZA BINADAMU

## Utangulizi

Kukosekana kwa uvumilivu wa kisiasa na kuchukua jukumu la kulinda na kukuza haki za binadamu ni masuala ambayo yaliendelea kuathiri haki za binadamu kwa mwaka 2018.

## 10.1. Uvumulivu wa Kisiasa

Mivutano na chuki za kisiasa ziliendelea kuonekana mwaka 2018, hasa kati ya wanachama na viongozi wa chama tawala na wale wa vyama vya upinzani, hususan kipindi cha chaguzi za marudio jijini Dar es Salaam na maendeo mengine ya Tanzania Bara kama vile mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Kigoma. Vurugu ziliripotiwa kutokea wakati wa chaguzi hizi na kupelekea majeraha mbalimbali kwa watu na baadhi ya wagombea. Pia, mwaka 2018 kulikuwa na mvutano miongoni mwa wanachama wa chama cha siasa cha CUF, kati wa wafuasi wa Prof. Ibrahim Lipumba na wa Seif Sharif Hamad. Mivutano hii, kati ya wanachama wa chama tawala na miongoni mwa wanachama wa chama cha CUF, pia ilitamalaki mitandaoni.

LHRC inaona kwamba mivutano hii na kupungua kwa uvumilivu wa kisiasa kunasababishwa na mambo kadhaa, ikiwemo uminywaji wa haki za msingi za binadamu kama vile uhuru wa kujieleza na uhuru wa kukusanyika, kinyume na Katiba na sheria za kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Kuna haja kwa Serikali, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, vyama vya siasa na wanajamii kwa ujumla kukaa pamoja kutatua changamoto zinazopelekea kupungua uvumilivu wa kisiasa na kukuza uvumilivu huo, hasa katika kipindi hichi ambacho Tanzania inaelekea katika chaguzi kubwa mbili za mwaka 2019 na mwaka 2020, ili tuweze kuwa na uchaguzi huru na wa amani.

## 10.2. Jukumu la Wadau Mbalimbali katika Kuendeleza, Kusimamia, Kuboresha na Kulinda Haki za Binadamu

Serikali zina jukumu la awali la kukuza na kulinda haki za binadamu katika sheria za nchi na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa na kutakiwa kutoingilia ufurahiaji wa haki hizo kinyume na sheria. Jukumu hili pia lipo kwa mtu mmoja mmoja, vikundi na vyombo vya mbalimbali katika jamii, kama inavyoelezewa na Umoja wa Mataifa kwenye tamko liitwalo "Tamko kuhusu Haki na Wajibu wa Mtu Mmoja Mmoja, Vikundi na Vyombo katika Jamii wa Kukuz na Kulinda Haki za Msingi za Binadamu zinazotambulika Duniani kote." Tamko hili linatoa haki ya kukuza haki za binadamu na kuelezea majukumu ya wadau katika kukuza na kulind haki za binadamu.

Wadau muhimu katika ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu ni pamoja na: wanasiasa; maafisa wa serikali; asasi za kiraia; viongozi wa dini; viongozi wa kimila; na maafisa wa vyombo vya dola. Watu wengine pia wana jukumu la kulinda na kukuza haki za binadamu; na hii inajumuisha kuingilia kati pale ambapo wanaona haki za binadamu zinakiukwa na kutoa taarifa kuhusu matukio hayo kwa mamlaka husika. Kila mwananchi ana jukumu la kutii sheria na kufuata taratibu za kisheria, pamoja na kutoa taarifa kuhusu matukio ya uhalifu na ukiukwaji wa haki za binadamu. Pia, ana jukumu la kuingilia kati kulinda haki za binadamu pale inapowezekana. Kwa mwaka 2018, bado wananchi walikuwa wazito kulifanyia kazi jukumu hili, hali iliyochangia kushamiri kwa vitendo vya ukatili na ukiukwaji wa haki za msingi za binadamu.

# MATATIZO YA JUMLA YANAYOATHIRI ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

- Sheria mbaya, zenye mapungufu au zilizopitwa na wakati, kinyume na viwango na kanuni za haki za binadamu
- Uelewa mdogo wa sheria, zikiwemo zinazohusu haki za binadamu, kwa pande zote
- Kukosekana kwa uwajibikaji binafasi na wa kitaasisi
- Kutofuata utaratibu wa kisheria
- Ufinyu wa bajeti katika sekta muhimu
- Rushwa na ukweapaji kodi
- Uvivu na imani za kishirikina
- Uelewa mdogo wa haki za binadamu baina ya wananchi na viongozi wao
- Ndoa na mimba za utotoni
- Kupungua kwa nafasi ya ushiriki

# MAPENDEKEZO MUHIMU

## HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

### Serikali

Serikali, kupitia Wizara ya Katiba, kutangaza rasmi kwamba imesitisha adhabu ya kifo na kufanya jitihada za kufanya marekebisho ya sheria kuondoa adhabu hiyo.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Jeshi la Polisi wahakikishe maaskari polisi wa ngazi zote wanapata mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Kanuni za Msingi za Umoja wa Mataifa kuhusu Matumizi ya Nguvu na Silaha ya Maafisa wa Vyombo vya Dola pamoja na mafunzo ya haki za binadamu kwa ujumla, kama njia mojawapo ya kushughulikia tatizo la mauaji yanayofanywa na maafisa wa vyombo hivyo.

Mhimili wa Mahakama na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kufanya kazi kwa karibu ili kutatua tatizo la rushwa katika mfumo wa utoaji haki na kurejesha imani ya umma kwenye vyombo vya usimamizi wa haki na kupunguza matukio ya kujuchukulia sheria mkononi na kuongeza upatikanji wa haki.

Serikali, kupitika Wizara ya Katiba na Sheria, kufanya marekebisho ya sheria ambazo zinaminya haki za ushiriki, hasa uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujumuika na uhuru wa kukusanyika. Sheira hizi ni pamoja na Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 ilioyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ifanye mapitio ya Kanuni za Maudhui ya Mtandao ili kuondoa au kurekebisha vifungu ambavyo havikidhi viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza.

Wakuu wa mikoa na wilaya wazingatie mipaka ya mamlaka yao ya kukamata na kuweka watu kizuizini chini ya Sheria ya Tawala za Mikoa na kutotumia vibaya mamlaka hayo.

Jeshi la Polisi kukemea vikali tabia ya baadhi ya maaskari polisi kuwabambikizia raia kesi, kukamata watu kinyume ana sheria na kuwaweka kizuizini watuhumiwa badala ya kuwafikisha mahakamani katika kipindi cha masaa 24 kama inavyotakiwa kisheria. Jeshi hilo pia liwachukulie hatua kali za kinidhamu na kisheria maaskari watakaojihusiha na vitendo hivyo.

Serikali kuridhia na kutungia sheria Mkataba dhidi ya Mateso na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Uteswaji).

Maafisa wa serikali na maaskari polisi kujiepusha na uingiliaji wa uhuru wa uhuru wa kukusanyika na kujumuika kinyume na sheria;

Serikali itie sahihi na kuridhia Mkata wa Afrika kuhusu Demokrasia na Utawala Bora wa mwaka 2007 ili kuimarisha ushiriki wa wananchi katika michakato ya kidemokrasia;

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa irekebishe vifungu vipya vilivyopitishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa kwa kufanyia kazi vifungu vyenye utata na vinavyominya uhuru wa kujumuika vilivyoainishwa na wadau mbalimbali;

Kuna haja ya kuwa na chombo huru cha kusimamia uwajibikaji na kuwachunguza maafisa wa vyombo vya dola wanaokiuka taratibu za kazi zao na sheria. Wadau wengine Asasi za kiraia ziongeze juhudi za kueneza uelewa wa umma kuhusu taratibu za kisheria na haki za kiraia na kisiasa, pamoja na kuwahamasisha wanajamii kutii sheria na kuheshimu haki za binadamu ili kulinda haki hizo, ikiwemo haki ya kuishi.

Asasi za kiraia zishirikiane kwa karibu na Tume ya Haki za Binadamu kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu haki za binadamu kwa majaji, mahakimu na wanataaluma wengine wa sheria ili kuwaongezea uelewa kuhusu haki za binadamu na nafasi yao katika kuzikuza na kuzilinda, ikiwemo haki ya usawa mbele ya sheria, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa haki.

## Wanajamii

Kujiepusha kujichukulia sheria mkononi na kutafuta nafuu za kisheria katika ngazi ya juu zaidi ya mfumo wa haki pale ambapo hawajafurahishwa na hukumu ya kesi.

Wanajamii pia wanatakiwa kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukiukwaji wa haki zao za kiraia na kisiasa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo ni taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu yenye mamlaka ya kulinda na kukuza haki za binadamu.

# HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI

## Serikali

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iongoze jitihada za kutatua migogoro ya ardhi na kuitafutia fumbuzi za kudumu ili kulinda haki ya kupata, kutumia na kumiliki mali na kukomesha mauaji yanayotokana na migogoro hiyo, hasa kati ya wakulima na wafugaji.

Wizara ya Kazi na Ajira ihakikishe kwamba Taratibu za Mishahara na Kanuni za Ajira zinafanyiwa mapitio mara kwa mara kama inavyotakiwa kisheria, ili kuhakikisha utekelezaji na ufurahiaji wa haki ya kufanya kazi na kukuza ujira.

Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, iongeze na uwekezaji kwenye umwagiliaji ili kuimarisha zaidi haki ya kufanya kazi kwenye sekta ya kilimo na kukuza uchumi.

Wizara ya Kazi na Ajira iimarishe mifumo ya ulinzi wa haki za kazi na kuhakikisha ukaguzi wa mahala pa kazi unafanyika mara kwa mara ili kuhakikksha haki zinaheshimiwa, kulindwa na kukuzwa, ikiwemo haki ya mazingira mazuri ya kazi.

Wizara ya Elimu na Ufundi ishirikiane na Wizara ya Kazi na Ajria na wadau mbalimbali kutafuta ufumbuzi wa tatizo la wahitimu wengi wa chuo kikuu kukosa stadi/sifa za kuajiriwa.

Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Ufundi, kutatua changamoto mbalimbali zinazoikumba sekta ya elimu, kama vile mazingira duni ya kufanyia kazi ya walimu na upungufu wa madarasa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Wizara ihakikishe nyumba za walimu zinajengwa na walimu wanalipwa mishahara kwa wakati.

Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, ifanye uwajibikaji wa makampuni kijamii kuwa takwa la kisheria katika sekta zote, baadaa ya marekebisho katika Sheria ya Madini mwaka 2017 kufanya suala hilo kuwa takwa la kisheria kwa upande wa makampuni yaliyo kwenye sekta ya madini.

Kuhusiana na wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni, LHRC inaiasa Serikali kufikiria upya na kubadilisha msimamo wake wa wanafunzi hao kutoruhusiwa kuendelea na masomo, ili kulinda haki ya ulimu kwa wasichana kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Wizara ya Elimu na Ufundi iongeze upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu (elimu jumuishi) kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu inayohitajika, walimu na vifaa vya kujifunzia.

Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwenye sekta muhimu za afya, elimu na maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, na maji.

Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo na kuongeza uwekezaji katika umwagiliaji ili kuimarisha haki ya chakula.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ihakikishe upatikanaji wa nyumba zilizo katika hali ya kufaa lakini kwa gharama nafuu kulingana na Dira ya Maendeleo ya 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuongeza juhudi za kudhibiti na kutatua tatizo la upotevu wa maji, wambao umekuwa ukisababisha hasara ya mabilioni ya fedha.

## Wadau wengine

Sekta binafsi ishirikiane na Serikali kuwekeza katika miradi ya maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma za maji. Hili linaweza kufanyika kama sehemu ya uwajibikaji wa makampuni kijamii.

Sekta binafsi na asasi za kiraia zinatakiwa kuisadia Serikali kutatua changamoto mbalimbali katika sekta za afya, elimu na maji, kama vile uhaba wa majengo na vifaa. Hii ni pamoja na ukarabati wa majengo na miundombinu, kama vile vyoo na madarasa.

Asasi za kiraia ziisaidie Serikali kutengeneza mikakati ya kutatua changamoto mbalimbali katika sekta za elimu, afya, maji na makazi, ili kukuza haki za kijamii na kiuchumi.

Asasi za kiraia kushirikiana na Wizara ya Kazi na Sheria kueneza uelewa kuhusu sheria za kazi, haki na wajibu, pamoja na haki za kiuchumi.

Wawekezaji wa ndani na nje wanatakiwa kufuata taratibu za kisheria kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji na kuheshimu haki za watu pamoja na kuzingatia sheria za nchi.

## Wanajamii

Umma ujenge tabia ya kutafuta maarifa na taarifa mbalimbali kuhusu haki zao za kiuchumi, ikiwemo haki ya kufanya kazi na haki ya kumiliki mali, ikiwemo matoleo ya lugha nyepesi ya sheria kuhusiana na haki hizi.

Wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukikuwaji wa haki za kiuchumi kwa mamlaka husika, ikiwemo vyama vya wafanyakazi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Wanajamii kuilinda miundombinu mbalimbali na kujiepusha na tabia ya kuiharibu, hasa miundombinu ya maji. Pia, wana jukumu la kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu matukio ya uharibifu wa miundombinu.

# HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

## Serikali

Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum kuhusu ukatili wa kijinsia.

Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria, kufanya mapitio na kuondoa au kurekebisha sheria zote zinazowabagua wanawake na kuwanyima haki zao kinyume na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania;

Serikali kuzingatia usawa wa kijinsia katika teuzi na nafasi mbalimbali za uongozi na utoaji maamuzi ili kuongeza uwakilishi wa wanawake.

Serikali kutimiza wajibu wake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto kufanya mabadiliko ya sheria ili kuondoa ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Jeshi la Polisi na Mhimili wa Mahakama kuongeza kasi ya uchunguzi na uendeshaji wa kesi za ukatili dhidi ya watoto.

Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge na Watu wenye Ulemavu kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapewa nafasi sawa katika soko la ajira kulingana na sheria.

Serikali, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, kuhakikisha kwamba wazee wanalindwa dhidi ya aina zote za ukatili, hasa mauaji yanahotokana na imani za kishirikina;

Serikali, kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuanzisha na kuendelea mchakato wa kutunga sheria ya haki za wazee.

Serikali, kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kutekeleza Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kulingana na Maoni ya Jumla Na. 21 kuhusu Watoto walio katika Mazingira ya Mtaani ya Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto, ili kulinda na kukuza haki za watoto wa mtaani.

## Wadau wengine

Asasi za kiraia zishirikiane na Serikali kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa Mkataba wa Haki za Mtoto ili kulinda haki za watoto wote, ikiwemo watoto wa mtaani na watoto wenye ulemavu.

Asasi za kiraia ziendelee kueneza uelewa kuhusu haki za wazee na kufanya kampeni za kupinga na kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wazee.

## Wanajamii

Wanajamii kutekeleza wajibu wao wa kuwalinda watoto na kuzilinda haki zao, pamoja na kujiepusha na vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto. Wanajamii kujiepusha na vitendo vya ubaguzi dhidi ya watoto, ikiwemo watoto wa mtaani na watoto wenye ulemavu.

Wanajamii kujiepusha na tabia ya kuwalinda watuhumiwa wa ukatili dhidi ya watoto kwa sababu tu ya kutaka 'kuficha aibu ya familia.

Wanawake na watoto watoe taarifa kuhusu matukio ya ukatili wanayofanyiwa na kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika ili sheria ichukue mkondo wake na wao wapate huduma na msaada wanaohitaji, ikiwemo huduma za kiafya na kisheria.



**Wakati unasoma ujumbe huu wapo watu wanateseka kwa kushindwa kufikia huduma za haki.**

Washike mkono,
jitolee kadri uwezavyo

## Jinsi ya kuchangia (Airtel Money)

Changia kwa Airtel Money
Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya Airtel Money (*150*60#)
Hatua ya 2: Chagua (5) Lipia Bili
Hatua ya 3: Chagua (4) Ingiza Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Ingiza Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Kiasi Unachotaka Kuchangia
Hatua ya 6: Ingiza Namba ya kumbukumbu (1234)
Hatua ya 7: Weka Namba ya Siri Kuthibitisha Muamala

## Jinsi ya kuchangia (TigoPesa)

Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya Tigo Pesa (*150*01#)
Hatua ya 2: Chagua (4) Lipia Bili
Hatua ya 3: Chagua (3) Ingiza Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Ingiza Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Kumbukumbu Namba (1234)
Hatua ya 6: Weka Kiasi Unachotaka Kuchangia
Hatua ya 7: Ingiza Namba ya Siri Kuthibitisha Muamala

## Jinsi ya kuchangia (M-Pesa)

Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya M-Pesa (*150*00#)
Hatua ya 2: Chagua (4) Lipa kwa Mpesa
Hatua ya 3: Chagua (4) Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Weka Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (1234)
Hatua ya 6: Weka Kiasi
Hatua ya 7: Weka Namba ya Siri
Hatua ya 8: Bonyeza 1 Kuthibitisha Muamala

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*

LHRC
LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

**Legal and Human Rights Centre (LHRC)**
Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam- Tanzania
**Tel:** +255 22 2773038/48; **Fax:** +255 22 2773037
**Email:** lhrc@humanrights.or.tz **Website:** www.humanrights.or.tz

**Arusha Office,**
Olerian Street, Plot No. 116/5, Sakina kwa Iddi
P.O. Box 15243, Arusha Tanzania
**Phone:** +255 27 2544187
**Email:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**The Legal Aid Clinic**
Isere Street – Kinondoni
P. O. Box 79633, Dar es Salaam – Tanzania
**Phone/ Fax:** +255 22 27612015/6
**Email:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz

Haki TV

***For a Just and Equitable Society***